


ANAYENG'ANG'ANIA

 Hebu tuendelee tu kusimama, kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi huku. . . Kabla hatujaenda kwenye maombi, kuna haja zozote ungetaka kufanya zijulikane kwa kuinua tu mkono wako? Nina hakika Yeye ataelewa kilicho chini ya mkono wako. Mungu na atujalie. Na tuinamishe mioyo yetu sasa mbele Zake.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunakukaribia tena, usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu kutoa shukrani na sifa kwa yote ambayo tumeona na kusikia siku nzima, na kwa ajili ya afya na nguvu zetu, kwa kuwa hai na duniani, na kukusanyika hapa usiku wa leo, katika kukuabudu Wewe.

³ Sasa, jalia Roho Mtakatifu mkuu aje miongoni mwetu usiku wa leo, Bwana, na kutenda tu miujiza na maajabu. Nasi tunaomba ya kwamba utatufanyia kama ulivyowafanyia wale huko Emau usiku ule, kwamba tutakapoondoka hapa usiku wa leo, jalia twende nyumbani tukisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Tujalie, Baba.

⁴ Bariiki kusomwa kwa Neno, na fungu na muktadha. Na ninii. . . Tunajikabidhi Kwako, Bwana, pamoja na Neno Lako, tutumie upendavyo. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁵ Bwana awabariki. Tunahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu sana, usiku wa leo, kukusanyika hapa pamoja nanyi tena katika maombi. Tumekuwa na siku nzuri sana. Nami kidogo nimepwelewa na sauti, ninahubiri wakati wote, na kwa hiyo mimi, ninadumu nimekorogwa kidogo kooni.

⁶ Lakini tulikuwa na mkutano mzuri asubuhi ya leo kwenye ushirika, ule mkutano wa Ushirika wa Wafanyabiashara kwenye Mkahawa wa Clifton, tulikuwa na wakati mzuri sana. Daima tunaufanyia huko kwa Clifton. Inashikilia kumbukumbu nyingi kwangu. Nami. . .

⁷ Kama mama yule yupo hapa aliyelipia kiamshakinywa changu asubuhi ya leo, Dada, ninataka kukushukuru. Hata sikumjua huyo mwanamke, aliingia na kuzunguka mbele yangu. Naye akaweka rubabu kidogo pale, kwa hiyo alijua nilikuwa mvulana wa mashambani, kwa hiyo akanipa rubabu. Ndipo nilipotoka, yule mhudumu alisema, ama, keshia alisema, “Yule mama ndio kwanza alipie chakula chako cha kutwa,” mimi, ama, “kiamshakinywa chako.” Sikujua alikuwa ni nani. Na kama yupo hapa, hakika ninataka kumshukuru.

⁸ Naam, tuna wakati mzuri sana asubuhi huko kwa Clifton, na Bwana amefanya mambo makuu. Ndugu Victor *Le Doux*, na—najua silitamki hilo vizuri, *Le Doux*, hapo ndipo unabii

ule ulipotokea kutoka kwa Danny Henry, ninao katika Biblia yangu hapa, ambalo lilikuwa ni jambo kuu. Wakati Danny Henry, mimi... alipokuja kunikumbatia kuomba pamoja nami, na, baada ya ibada, naye alinena katika Kifaransa. Na—na ikawa mkalimani wa U.N. alikuwa humo jengoni na kufasiri. Na ilikuwa ndicho kitu hasa nilichokuwa nikitafuta kutoka kwa Mungu. Na kwa hiyo, mambo mengi.

⁹ Nami ninakumbuka jambo moja. Hili kwa namna fulani ni kwa ajili ya, inawafaa nyinyi akina dada, mwajua. Wao... Nilikuwa nimesimama nikimngojea Ndugu Arganbright, ndugu yangu wa thamani katika tawi la Wafanyabiashara wa Full Gospel kule, na—naye alikuwa anaingia. Wala kamwe sikuwa nimeona chochote cha vitu hivi vipya ambavyo wanawake wanavaa usoni mwao. Ndipo nikamwona mwanamke akija pale akiwa na macho ya kijanikibichi, na mwekundu kote na usoni mwake, nami ni—nikawazia, “Maskini mwanamke huyo!” Nikaangalia nyuma, nami nikawazia... Mimi—mimi ni mmishenari, na ni—ni—nimeona upele na nimeona ukoma, bali si—sikujua alikuwa na shida gani. Nami nikaandelea kusimama, nikiangalia, nikawazia, “Unajua, ni—ninaamini nitaenda kule na kumwambia maskini huyo mwanamke, ‘Mimi...’ Nilikuwa nikitaka kwenda na kusema, “Dada, samahani. Mimi—mimi—mimi huwaombea wagonjwa, kama—kama kuna—kama kuna jambo lolote ninaloweza kufanya kukusaidia, nijulishe.”

¹⁰ Ndipo huyu hapa akaja mwanamke mwingine, vivyo hivyo, nikasema, “Hapana shaka, labda wana namna fulani ya maonyesho, mwajua, ama kitu fulani wanachojipaka,” wachekeshaji, mwajua, jinsi wanavyojipaka rangi, mwajua, na kuonekana hivyo. Na kwa kawaida nisingefikiri mwanadamu angetaka kujiharibu sura namna hiyo, mimi... mwanamke mrembo angetaka kuonekana hivyo.

¹¹ Ndipo basi walikuwa na mtindo huo mkubwa wa kukata nywele kichwa-maji, mwajua, namna hiyo ya... na hakika, ulikuwa ni mwonekano mbaya sana... Lakini msichana mrembo amesimama pale, na kuchafua ninii yake... Vema, jambo ni kwamba, ni wazo hilo la Mama Taifa, mwajua. Nanyi mwajua, Yezebeli alikuwa mama taifa wa—wa Palestina wakati mmoja, pia, kwa hiyo kuwa mwangalifu kile unachoiga, unaona? Usijaribu... Jaribu kuonekana kama Mungu alivyosema. Achilia nywele zako zikue, hivyo ndivyo Mungu alivyosema ufanye.

¹² Ile siku baada ya mikutano yetu huko Phoenix kulikuwako na maskini mama mmoja aliyekuja, kasema, “Ndugu Branham, tangu ile mikutano,” kasema, “ninaachilia nywele zangu zikue.”

Nikasema, “Huko mbali na Ufalme sasa.”

¹³ A—akasema, “Dada yangu alikuwa na toroli iliyojaa kaptura hizi na kadhalika, alikuwa anaenda kuzitupa kwenye pipa la

takataka, ndipo dada anayefuata akaja, akazichukua.” Kisha kasema, “Alisema alikuwa amemalizana na vitu hivyo.”

Kwa hiyo nikasema, “Hilo ni sawa, ninaamini Kanisa litasimama tena siku moja, kama likiendelea hivyo, litakuwa sawa.”

Nilikutana na mtu si muda mrefu uliopita, akasema, “Kwa nini usiwaache wanawake hao?”

Nikasema, “Vema, sijui.”

Akasema, “Watu wanakuchukulia kama nabii.”

Nikasema, “Mimi siye.”

Akasema, “Lakini wanakuchukulia hivyo. Kwa nini usiwafundishe mambo yenye kilindi, jinsi ya kupokea karama zenye kilindi za kiroho?”

¹⁴ Nikasema, “Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawatajua ABC zao?” Mnajua *ABC* inasimamia nini, sivyo? “Daima Mwamini Kristo.” [Kiingereza: “Always Believe Christ”—Mfa.] Na hiyo—hiyo ni kweli, hizo ndizo ABC za kwanza. Acha wajifunze jinsi ya kufanya hilo, ndiposa tutafundisha jambo fulani tofauti kidogo, mwajua. Na kwa hiyo, tunapopata hilo, mbona, tunakuja karibu sana na—na Ufalme.

¹⁵ Sasa, imekuwa ni siku kuu. Nilikuwa na wakati mzuri sana hapa jana usiku. Aisee, mwajua, mlijaribu baadhi ya sumu hiyo? Ni sawa, sivyo? Mwajua, Petro aliwaambia jinsi ya kuchanjwa. Nanyi mnajua walifanya mambo ya kiajabu, bali hakika walikuwa wamechanjwa, hilo lilikuwa jambo moja.

¹⁶ Tulikuwa, wakati tungewapiga ndama chapa, mwajua, tungechukua chuma cha kutia alama, na kukiweka juu yao kwa kishindo namna *hiyo*, na jamani, mnazungumza juu ya kulia na kupiga mayowe, bali yeye alijua ni wa nani baada ya hapo, hilo lilikuwa jambo moja kwake. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo, huenda akakufanya upaze sauti kidogo, bali unajua mahali ulipo baada ya hayo. Hiyo ni kweli. Wewe ni ukoo safi tangu wakati huo na kuendelea.

¹⁷ Chochote nisichokipenda ni—ni ucho tara. Nilihubiri juu ya hilo siku moja, na daima nilisema kimoja cha vitu vibaya sana ni nyumbu. Jamaa huyo hajui baba, mama ni nani, hajui alikotoka, na hakika haendi popote, maana yeye, mnaona, mama yake, fa—farasi na baba yake, pu—punda, na—na yeye ni—yeye ni . . .

¹⁸ Hiyo inathibitisha sayansi, wakati wanapowazia ya kwamba watu waliendelea kuwa wakubwa zaidi na kuzalishana, na kadhalika, kutoka kwa uhai wa wanyama kwenda juu, mbona, mara ya kwanza unapochanganya mbegu, inaikomesha papo hapo, haiwezi kuendelea mbele zaidi. U—unaweza kufanya mahindi chotara, bali huwezi kupanda hayo mahindi chotara tena, hayatakua. Kwa hiyo mnaona, ndio kwanza wa—

wamegundua hilo jambo lilihukumu nadharia yao wenyewe, kwa hiyo huwezi kufanya hivyo.

¹⁹ Kwa hiyo...Lakini mimi...Nyumbu, yeye ni bubu, mwajua, ungeweza tu kuzungumza naye, naye atangojea maishani mwake mwote apate, kukupiga teke kabla hajafa. Naye...Unaweza kumwambia...Huwezi kumfundisha chochote, ana kichwa kigumu. Unaweza kujaribu kuwa mpole kwake, naye atayanyoosha masikio yake, mwajua, na kupiga makelele, "Hoo, siku za miujiza zimepita. Hoo, hakuna kitu kama hicho," nanyi mwajua, akilia tu kwa sauti kali.

²⁰ Lakini farasi mzuri, ukoo safi, unaweza tu kumfundisha chochote. Anajua baba yake ni nani, mama yake ni nani, baba wa babu yake na mama wa nyanya yake, anajua historia huko nyuma kabisa.

²¹ Vivyo hivyo na Mkristo mzuri ukoo safi aliyezaliwa na Roho Mtakatifu. Haimbidi kusema, "Nilikuwa Mmethodisti, Mbaptisti, na ilinibidi kubadilika nikawa Mpresbiteri, Mlutheri." Alizaliwa na Roho Mtakatifu katika familia ya Mungu, na ukoo safi unaenda moja kwa moja pamoja nayo hadi Pentekoste. Haleluya! Amina. Ninapenda chanjo hiyo.

²² Nilishangazwa na Dada Shakarian. Uko hapa, Dada Shakarian? Dada Demos Shakarian, asubuhi ya leo alikuwa akisimulia mkutanoni kwenye...Phoenix tulikuwa na dhifa, chakula cha kutwa, dhifa, ama chochote mnachokiita, ninachanganyikiwa na hicho wakati wote. Ni—nilikuwa na kiamshakinywa, na chakula cha kutwa, na chakula cha jioni, na sasa, wana chakula hicho cha kutwa kilichowekwa hapa kama chakula cha jioni, basi kama nikiita hicho chakula cha kutwa, basi itakuwaje kwa chakula changu cha jioni? Kamwe siwezi, siwezi kunyoosha jambo hilo kwa namna fulani. Na—nami...ni kiamshakinywa tu, chakula cha kutwa, na cha jioni nyumbani kwetu, kwa hiyo basi hilo ni sawa. Unaninii...huli chakula cha kutwa cha Bwana, unakula chakula Chake cha jioni. Hiyo si ni kweli? Bwana...Kwa hiyo tuko moja kwa moja kwenye hilo, ndugu, yeyote aliyesema, "Amina," kwa hilo.

²³ Lakini tulikuwa tukifanya dhifa hiyo usiku huo, na ikatokea kuwa...Huna mamlaka juu ya kile Roho Mtakatifu atakachofanya. Unaona? Humtawali, Yeye anakutawala, unaona. Mtu yeyote anapoingia, kasema, "Sasa, wewe, *nani*..." Mbona, hujui atakalofanya, inakubidi tu kungojea.

²⁴ Ndipo ninakumbuka, Roho Mtakatifu alishuka. Na—na kwenye upambanuzi huo, ni kama tu kuingiza gia. Nao watu hawatambui jambo hilo, bali wao ndio wanaofanya hivyo, si mimi, ni imani yao wenyewe.

²⁵ Huenda nikajaribu kutoa maelezo yake kwa dakika moja tu au mbili, kujaribu kulieleza. Huwezi kumfafanua Mungu, kwa sababu inakubidi tu kumwamini Mungu. Kama unaweza

kumfafanua, basi huwezi tena kulikubali kwa imani, unaona, kwa sababu unajua yote kulihusu, kama unaweza kulifafanua. Lakini tunamkubali Mungu kwa imani.

²⁶ Lakini mnaona, katika Kristo mlilika utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Sasa, Yeye alikuwa ni Mungu, sisi ni sehemu ya huyo Roho. Tulipewa kwa kipimo, Yeye bila kipimo. Lakini kama nilichota kijiko kimoja cha maji, ama kikombe cha maji, kutoka baharini hapa nje, kungekuwa na kemikali zile zile katika maji hayo, kama zilizo katika bahari yote.

Kwa hiyo hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo. Anapokuwa ndani yetu si mkubwa hivyo, bali ni—ni katika . . . Ni Roho yeye yule tu, anafanya mambo yale yale.

²⁷ Ndipo mnaona wakati mmoja wakati Bwana wetu . . . Yeye alisema hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha Yeye kwanza. Naye alikuwa na rafiki aliyetwa Lazaro, Naye, akiishi na rafiki huyu, naye rafiki huyo alikuwa anaenda kuwa mgonjwa, kwa hiyo hapana shaka Baba alimwita aondoke, na akampa ono aondoke.

²⁸ Alingojea siku *kadhaa*. Wakaagizia aitwe, Yeye kamwe hakwenda, Yeye aliendelea tu na safari. Ndipo baada ya wakati ufaao ambao Baba alikuwa amemwonyesha ingemchukua Lazaro kufa, Yeye alisema, “Lazaro amekufa. Na kwa ajili yenu nina furaha sikuwapo, lakini ninaenda kumwamsha.”

²⁹ Na kwa hiyo, wakati alipokuja kwa ninii . . . Martha na hao wengine . . . Tunajua hadithi hiyo. Halafu basi, wakati alipomfufua mtu huyu aliyekufa, hakusema lolote kuhusu kuwa dhaifu, huyo alikuwa ni Mungu akitumia karama Yake.

³⁰ Lakini basi, maskini mwanamke mmoja alijipenyeza katikati ya umati na kugusa upindo wa vazi Lake, naye akageuka, bila kujua alikuwa ni nani, akasema, “Ni nani aliyenigusa?”

³¹ Naye Petro akamkemea, akasema, “Bwana,” kwa maneno mengine, huenda alisema hivi, “mbona, hilo linasikika lisilo la kawaida sana kwa—kwako Wewe kusema hivyo, wakati kila mtu anakugusa.”

³² Akasema, “Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu.” Ndipo akaangalia kila mahali mpaka akamwona huyo mwanamke, Naye akamwambia ya kwamba kutokwa kwake na damu, kwamba imani yake ilikuwa imemwoko, imani yake, si maombi Yake, imani Yake, bali imani ya mwanamke huyo. Hiyo ilikuwa ni huyo mwanamke akimgusa Mungu kupitia Kwake iliyomdhoofisha. Hiyo ilikuwa ni huyo mwanamke akitumia karama ya Mungu, bali wakati Mungu alipoitumia karama Yake Mwenyewe, hakusema lolote kulihusu, mnaona, kuwa mnyonge.

³³ Vema, hivyo ndivyo ilivyo mikutanoni, ni watu wanaofanya hivyo. Kama huliamini, halitafanikiwa kamwe, imani yako

ndiyo inayolifanya, na kwa hiyo, hilo ndilo linalosababisha hayo mambo kutukia katika kusanyiko jinsi yafanyavyo.

³⁴ Basi usiku huo wakati tulipokuwa kwenye dhifa, Roho Mtakatifu alianza kutembea kwenye kusanyiko na kuzungumza na watu mbalimbali, na kuwaambia. Nami nikaona nyuma yangu kulikuwa na mwanamke mkongwe amesimama upande *huu*, kama tu kuangalia kwenye skrini ya televisheni akiliangalia likitendeka, kisha kusema tu kile unachoangalia, jambo lile lile tu, ni kwamba unaangalia kitu fulani. Ni kama tu vile ulikuwa umelala na kuota, ila tu hujalala, unakiangalia tu. Ni kiwango kingine, na unashuka chini kabisa, yale yamekuwa, na mbali sana, yale yatakayokuwa. Huyu ni Mungu akifanya hivyo.

³⁵ Ndipo nikaona nyuma yangu, na ilionekana kana kwamba ilikuwa ikitoka kule pembeni, kama ambapo yule mama ameketi *pale*. Nami nikaangalia huko nyuma, na ilikuwa ni Dada Shakarian, nami nikawazia, “Huyo siye.” Ndipo nikaangalia nyuma, na huyu hapa mama amesimama hapa, nami nikaona mtoto wa jicho ukiingia jichoni mwake. Ndipo nikaangalia tena, wala haikuwa. . . Nilijua alikuwa ni mkongwe sana asingekuwa ni Dada Shakarian, haikuwa na upendeleo hata kidogo. Ndipo nikawazia, “Kama nikizungumza naye basi ono litakuja, kama anamwomba mtu fulani.”

³⁶ Basi jambo ni kwamba, mtaalamu huyu mashuhuri wa magonjwa ya moyo kutoka Pwani ya Magharibi hapa, ambaye ni daktari wa Ndugu Shakarian, walikuwa naye kule mkutanoni, yeye ni Seventh Day Adventist kwa dini, kwa madhehebu. Naye Bibi Shakarian alikuwa akiomba kwa bidii kwamba jambo fulani litukie, kwamba daktari angeweza kushawishika kwamba ilikuwa ni Mungu. Naye alikuwa ni daktari wa mama yake, ambaye alikuwa ameona ugonjwa wa mtoto wa jicho ukilifunika jicho lake.

³⁷ Na huyo hapo daktari ameketi pale, naye Bibi Shakarian hapa kwenye. . . ambapo alikuwa nyuma yangu, hakukuwa na mtu mwingine nyuma ya Bibi Shakarian, naye alikuwa ameketi pale akiomba, “Bwana, jalia jambo fulani litukie, sasa wakati upambanuzi unapoendelea, ambalo litamshawishi daktari huyu, apate kumpokea Roho Mtakatifu, yeye ni mtu mashuhuri sana.” Na kwa hiyo yeye. . .

³⁸ Ikasema, “Bibi Shakarian, unamwomba mama yako, na ugonjwa wa mtoto wa jicho unakuja juu ya jicho lake, naye anaingia upofu.” Lakini kasema, “Ninaona ukungu mweupe ukitoka kwa mama yako sasa, ukitoweka, ‘BWANA ASEMA HIVI,’ huo ugonjwa wa mtoto wa jicho utatoweka.”

³⁹ Ndipo akampigia simu mama yake, na kumwambia kesho yake. Katika siku chache, kila chembe ya huo ugonjwa wa mtoto wa jicho ilikuwa imetoweka, mama yake alikuwa mzima na mwenye afya. Naye daktari aliyemchunguza mwanamke huyo

na kuona ugonjwa wa mtoto wa jicho kwenye macho yake, akachunguza tena, nao ugonjwa wa mtoto wa jicho ulikuwa umetoweka. Ndivyo ilivyokuwa, huo. . .

⁴⁰ Kwa hiyo inaonyesha ya kwamba Mungu wetu angali ni Mungu. Yeye ni ninii tu. . . Na hivi hatuna furaha, usiku wa leo, kujua kwamba tuna Baba wa Mbinguni anayeweza kuondoa magonjwa ya mtoto wa jicho, kuondoa magonjwa? Naye ni Mungu tu, hivyo tu. Kwa hiyo tutazungumza Naye katika dakika chache kabla hatujasoma Neno Lake, kwa kuwa tumekuwa tukizungumza jinsi ambavyo tumezungumza, kisha tuzungumze usiku wa leo.

⁴¹ Na sasa, kesho alasiri ni ibada, kwa hiyo ndugu zetu wote na wote, kila mtu anaweza kurudi kanisani mwao. Sasa, asubuhi. . . Kuna makanisa kadhaa hapa yaliyowakilishwa, huu, udhamini wangu wa mkutano huu. Sasa, watu hawa wanaamini katika aina hii ya huduma, la sivyo wasingekuwa wakinidhamini na kuketi hapa karibu nami. Na kila mgeni yupo hapa, ambaye hana kanisa lao wenyewe hapa, mahali fulani wanapohudhuria, mbona usimwone mmoja wa hawa ndugu hapa, nadhani walisema walikotoka, kisha uhudhurie ibada zao asubuhi? Nina hakika watawanufaisha.

⁴² Na ni shauku yangu aminifu kwamba—kwamba mahali fulani kati ya hapa na kesho alasiri, kutazuka uamsho wa mtindo wa kale miongoni mwa makanisa haya hapa ambao utakuwa tu wenye utukufu na kwa ajili ya siku hii ya mwisho. Tunajaribu kupanda mbegu, kusudi Roho Mtakatifu atakaposhuka, atashuka juu ya kitu sahihi, atazaa aina nzuri ya zao, tunapotarajia ninii. . . siku hizi za mwisho.

⁴³ Basi kesho alasiri ndiyo ibada zetu za kufunga hapa. Na ndipo tuanzie huko, nafikiri kunaitwa Santa Maria. (Hiyo ni. . . ?) [Ndugu mmoja anasema, “Santa Maria.”—Mh.] Santa Maria. Kisha tunaenda kutoka huko hadi Grass Valley, halafu basi—halafu basi, kuendelea, na kuendelea, na kuendelea kupanda juu. Kwa hiyo basi, Bwana akipenda, ninapaswa kuwa katika. . .

⁴⁴ Ndugu Williams, uko hapa? Alikuwa—alikuwa. . . Ndugu Williams, ninii sana. . . Naam, Ndugu Williams anajaribu. . . kasema alifanya Phoenix yote iniombe, kwamba badala ya kwenda Tanganyika, na Kenya, na Uganda, na kote kupitia Afrika Kusini Januari hii ijayo, Februari, Machi, na Aprili, alikuwa akitaka kuomba ya kwamba tungekuwa huko Phoenix. Naye Ndugu Carl, ni—nitaenda tu jinsi anavyoniongoza, mnajua hilo, mnajua hilo. Bwana awabariki. Asanteni sana kwa uaminifu huo.

⁴⁵ Nami natumaini sasa, kesho alasiri, ya kwamba kila mtu atatokea, nasi tuna mkutano mkubwa kesho jioni. Ninajaribu

kuhubiri kidogo, kama sauti yangu inaweza, nasi tunatarajia wakati mzuri sana kesho.

⁴⁶ Sasa, ningetaka kusoma baadhi—baadhi ya Neno la thamani hapa. Nami ninawatakeni mfungue, kama mnafuatilia kwa makini, kama tunavyoliita huko kusini, fungu tungalosoma. Ningetaka... Nina muhtasari ulioandikwa hapa, Maandiko kadhaa. Ningetaka kufundisha kidogo tu, usiku wa leo, juu ya somo linalopatikana katika Mathayo Mtakatifu, mlango wa 15, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 21. Mathayo Mtakatifu, mlango wa 15 na kuanzia kifungu cha 21.

Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro ya Sidoni.

Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu, Ee Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo.

Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu.

Akakajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.

Naye akaja akamsujudia, akisema, Bwana, nisaidie.

Lakini akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.

Akasema, Kweli, Bwana: lakini hata mbwa hula... makombo yaangukayo kutoka mezani pa bwana zao.

Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Ee Mama, imani yako ni kubwa: na iwe kwake kama utakavyo. Ndipo binti yake akapona tangu saa ile.

⁴⁷ Kama lingelitwa somo, ningetaka kuchukua neno moja kwa ajili ya somo, na hilo ni neno *Anayeng'ang'ania*. *Anayeng'ang'ania*, Webster inasema, ni “kushikilia, kushikilia katika kutimiza lengo; kufanya jambo fulani.” Kung'ang'ania ni kushikilia, na kabla ya kushikilia inakubidi kuwa na fununu ya kile unachoshikilia.

⁴⁸ Na watu katika nyakati zote ambao wamewahi kujaribu kufanikisha jambo fulani wamekuwa wakishikilia. Mwanadamu, ili kushikilia, huenda nikanukuu tena, ni kujua kile unachotafuta. Na kama hujui, huna hakika na msimamo wako, lakini unapofahamu kabisa ni nini, kile unachotafuta, na umeridhika utafanya hivyo, basi unaweza kushikilia, ung'ang'anie kweli kweli, kushikilia.

⁴⁹ Ninapenda hu—huo mtazamo. Ninapenda watu wanaoshikilia wakati wanaponinii... tambua... haidhuru kama mtu huyo a—amekosea, bali hata hivyo anaamini kwamba

yuko sahihi. Lakini sasa, anapofikia mahali amethibitika kuwa amekosea, basi kujaribu kung'a- . . . hawezi kung'ang'ania basi, kwa sababu imethibitika kuwa amekosea, lakini wakati akiwa—akiwa sahihi, ndipo basi atalishikilia.

⁵⁰ Ninawazia usiku wa leo, juu ya rais mashuhuri wa kwanza wa taifa hili kuu tunayemthamini sana usiku wa leo, hii Marekani kuu, George Washington, mtu mashuhuri wa imani, mtu wa maombi, mtu mwenye kung'ang'ania, anayeng'ang'ania sana. Naye alijua alichokuwa akitafuta, basi usiku mmoja aliomba karibu usiku kucha, wakati yeye. . . ilionekana kana kwamba mambo yalikuwa magumu kwake. Naye akaomba mpaka akasema karibu mwili wake wote ulikuwa umelowa maji kutokana na kupiga magoti kwenye theluji, mpaka akapata jibu kutoka kwa Mungu.

⁵¹ Basi kesho yake asubuhi, huku nusu ya jeshi lake likiwa halina hata viatu miguuni mwao, hao walikuwa ni askari wa Marekani wasio na viatu, miguu yao imefungwa kwa matambara, Delaware uliganda kwenye makorongo ya barafu, alishikilia kwamba angeweza kuvuka Delaware, kwa kuwa alikuwa amesikia kutoka kwa Mungu. Haidhuru upinzani ulikuwaje, alikuwa amesikia kutoka kwa Mungu. Ingawa risasi tatu za gobori zilipitia kwenye koti lake, hakuna kitu kilichomgusa. Mbona, alishikilia kwa sababu alijua alikuwa sahihi, na mafanikio yake aliyokuwa akiyatarajia yalikuwa kwa ajili ya jambo sahihi!

⁵² Haidhuru watu hao walikuwa katika hali gani, jinsi miguu yao ilivyokuwa baridi, angeweza kushikilia, kwa sababu alijua alikuwa akijaribu kufanikisha jambo fulani kumsaidia mtu mwingine. Naye alikuwa ameomba mpaka akasikia kutoka kwa Mungu, naye akavuka Delaware katika wakati wa barafu.

⁵³ Huenda nikavuta usikivu wenu kwa dakika chache kwa mtu mwingine ambaye angeweza kung'ang'ania. Na mtu yeyote anaweza, wakati unajua kile unachozungumzia. Wakati mtu hajui wanachozungumzia, basi hawajui wapitie njia gani. Hiyo ndiyo sababu ninafikiri kwamba kama Ukristo na kikomo chako cha Milele vinategemea imani yako katika Mungu, afadhali ujue kama uko sahihi au la.

⁵⁴ Nuhu, mtu mashuhuri, ningetaka kuzungumza juu yake kwa dakika chache. Alitoka katika ukoo wa Sethi. Kama ukiangalia, ukoo wa—wa watoto wa Hamu wote walikuwa vipeo vikuu, walikuwa wanasayansi, watu mashuhuri, wasomi, wavumbuzi, na watu mashuhuri waliopitia kwa Kaini. Lakini kupitia upande huo mwingine wakaja watoto wa Sethi, walikuwa wachunga kondoo, wakulima wadogo, bali ni wa kidini halisi waliomtumikia Bwana na kumwamini Yeye.

⁵⁵ Basi siku moja wakati Nuhu, labda mkulima, huko nje kondeni (Ulimwengu ulikuwa mwovu kama ulivyo siku hizi,

mpaka kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya, na hata ikamhuzunisha Mungu kwamba alimwumba mwanadamu.), basi Mungu akanena na mkulima huyu mnyenyekevu na kumwambia ya kwamba atauangamiza ulimwengu kwa maji. Sasa, kamwe hakukuwa kumewahi kunyesha.

⁵⁶ Sasa, huo ulikuwa ni ujumbe wa jinsi gani kwa wakati wa kisayansi! Ndipo wakati. . . Wanadai sasa ya kwamba sayansi yetu ya siku hizi haitalingana na hao wa siku hiyo. Walijenga piramidi, tusingeweza kufanya hivyo leo, hatuna nguvu za kuinua miamba hiyo huko juu. Nao walikuwa na. . . Wangeweza kutia maiti dawa isioze huku ikionekana ya kawaida hata leo, hatuna siri hiyo ya kuhifadhi maiti walivyokuwa nayo wakati huo kufanya mumiani. Kutia rangi, na vitu vingi walivyokuwa navyo wakati huo ambavyo hatuna sasa. Na ni wakati wa kisayansi wa jinsi gani!

⁵⁷ Je, ungeweza kuwazia mtu akipanda kwenda kule, akiichukua familia yake na kujenga safina, na kusema ya kwamba kutanyesha maji kutoka mbinguni, wakati hakukuwa kumewahi kuwa na tone la maji lililoanguka kutoka angani? Ungeweza kuwazia vi—vicheko na dhihaka zilizomjia mtu huyo siku hizo? Jinsi ambavyo wanasayansi wangeninii. . . *Sayansi* ingekuja na kusema, “Angalia hapa, tuna chombo tunachoweza kurusha moja kwa moja hata kwenye mwezi na nyota, wala hakuna maji yoyote huko juu. Yanatoka wapi? Yatakuwaje huko? Nionyeshe mahali yalipo.” Neno la Mungu halikustahimili vipimo vyao vya kisayansi; wala halivistahimili siku hizi, bali tunaliamini kwa vyovyote vile.

⁵⁸ Naye Nuhu alishikilia, akang’ang’ania sana. Ninaweza kuwawazia wakiwachukua madaktari na kumleta mbele ya wataalamu wa magonjwa ya akili wapate kujua akili ya mzee huyo ina shida gani. Lakini haikuwa ni akili yake, ilikuwa moyoni mwake. Naye alikuwa na Neno la Bwana, naye alijua ya kwamba Huyu alikuwa ni Mungu.

⁵⁹ Nami ninaweza kumsikia Nuhu akisema, “Tkiwa hakuna maji huko juu, na Mungu alisema kutanyesha maji kutoka huko juu, Mungu anaweza kuweka maji huko juu.” Nayo hadithi yake ikashikilia kwa muda wa miaka mia moja na ishirini, wakati akijenga safina, akishikilia sana. Wakati wa wenye kudhihakiki hakuna aliyemsikiliza, bali walimcheka na kumdhihakiki kila mahali alipokwenda, lakini hata hivyo alishikilia moja kwa moja, kwa sababu alijua lilikuwa ni Neno la Bwana, alikuwa na hakika nalo.

⁶⁰ Ninaweza kuwazia, wakati mikutano yake ya mtaani ilipoanza, jinsi walivyocheke! Loo, walikuwa wa kidini wakati huo, kumbukeni, wa kidini sana, vivyo hivyo na Kaini, naye akajenga madhabahu kama vile Habili alivyojenga. Yeye. . . Kama—kama dini ndiyo yote Mungu anayohitaji, Yeye alikuwa

katili kumhukumu Kaini, maana Kaini alifanya kila tendo la kidini ambalo Habili alifanya, bali alikuja kwa njia mbaya. “Iko njia ionekanayo kuwa sawa, lakini mwisho wake ni njia ya mauti.”

⁶¹ Lakini sasa, huna budi kuwa na hakika ya kwamba uko sahihi, kwa hiyo kamwe hatuwezi kubahatisha tu juu ya hili. Hakuna haja ya kufanya hivyo, Kristo ameacha ki-kielelezo dhahiri sana hata sisi... Alisema hata mpumbavu hapaswi kukosea, mnajua kama ni kweli ama si kweli. Halafu basi, unapokuwa na hakika uko sahihi, sahihi Kimaandiko, basi unaweza kusimama pale kwa sababu... na kushikilia sana.

⁶² Sasa, Nuhu na mahubiri yake, jinsi ambavyo hapana shaka mtu fulani alisema, “Mzee yule kule juu angali anapiga nyundo ule mtumbwi.” Nao waliamini ya kwamba maskini mashua yoyote ingefaa kama ingenyesha mvua, iwe iliundwa na Mungu au la.

⁶³ Na hivyo ndivyo wanavyowazia siku hizi, maskini kanisa lolote litafaa, maskini wazo lolote la kidini. Nenda ukajiunge na *hili*, usipolipenda, nao hawapendi kule, nenda kwenye hilo lingine, lingine, lolote la hayo litafaa. Lakini Mungu ana Kanisa lililojengwa ambalo limejengwa juu ya Mwamba, Kristo Yesu, na “Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao,” alisema Eddie Perronet. Na hiyo ni kweli.

⁶⁴ “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.” Kanisa Katoliki lilisema ilikuwa ni juu ya Petro, akarudi nyuma baada ya hapo. Mprotestanti alisema ilikuwa juu ya Yesu, sikubaliani nanyi, Yeye alisema, “Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili.” Basi ilikuwa ni juu ya mwamba wa ufunuo wa kiroho wa Neno. Kweli.

⁶⁵ Jambo lile lile alilokuwa nalo Habili, jinsi lilivyofunuliwa kwake, badala ya kutoa tunda kama Kaini alivyofanya, alitoa damu, kwa kuwa ilifunuliwa kwake. Kanisa lote la Mungu limejengwa juu ya ufunuo wa kiroho wa Kristo, kwamba Yeye ni Nani, kile alichu, na yote kumhusu.

⁶⁶ Na sasa, tunaona ya kwamba Nuhu alidumu moja kwa moja na somo lake. Nami naweza kumwazia Mungu, siku moja, alitosheka na kucheka kwao na kumdhihaki Nuhu. Mnajua, Mungu anaweza tu kwenda, avumilie kiasi fulani, na halafu subira Yake inaisha. Kwa hiyo yalimtoha, Naye alikuwa anataka kufanya jambo fulani kwake, Naye akamwambia Nuhu, “Panda huko juu, na unawaona wanyama wakiingia katika safina? Wewe ingia moja kwa moja baada ya wanyama wote kuingia, nao mlango utafungwa nyuma yako.”

⁶⁷ Basi asubuhi hiyo wanyama wakaanza kuingia wawili wawili. Nami ninaweza kuwazia wenye kudhihaki wote wakismama huku wakisema, “Sasa, nendeni kule juu mkaishi na wanyama wenu wanaonuka. Ingieni mle ndani na mfunge

mlango pamoja na huo uvundo wote, na kadhalika, pamoja na wanyama hao.”

⁶⁸ Hivyo ndivyo wanavyojaribu kulisema tena siku hizi. Lakini mtu ambaye . . . anajua Safina ni nini, haidhuru inafanyiwa dhihaka kiasi gani, inahukumiwa jinsi gani ama yote kuihusu, mtu huyo anajua ya kwamba anaongozwa na Mungu. Kweli. Nuhu aliingia ndani ya safina, na mkono mkuu wa Mungu, wenye nguvu ukafunga mlango nyuma yake.

⁶⁹ Sasa, ninaweza kuwazia ya kwamba, wao walipoona jambo hilo, kulikuwako na watu ambao kwa namna fulani walikuwa ni mwaminio mkwamia mpakani, kasema, “Mnajua nini? Huenda ikawa huyo mzee alikuwa sahihi.” Ni wale tu wanaokaa mkutanoni, mwajua, na wanahudhuria kila mkutano (Nao wakasema, “Yule mzee . . .”), bali kamwe hawataki kuingia, kamwe hawako tayari kulikubali.

⁷⁰ Halafu, kama vile Waebrania 6 ilivyosema, na kama vile katika waaminio wakwamia mpakani wa Agano la Kale, daima wanaangalia tu, na kuangalia huku na huku, na kamwe wasiweze kuufikia ujuzi wa ile kweli, hawa hapa watu hawa wanakuja, na kusimama karibu, “Vema, maji yakianza kushuka kutoka kule, tutapanda na kubisha mlango, na kama mzee mwenye moyo mwema, yeye atafungua mlango na kuturuhusu kuingia. Kwa hiyo tutakaa hapa tuone kama mvua inakuja.”

⁷¹ Ninaweza kuwazia Nuhu akipanda kupitia orofa ya kwanza, akapanda juu, orofa ya pili, kisha akapanda hadi orofa ya tatu, akaja kupitia wakati wa Kilutheri, akarudi kupitia wakati wa Wesley, akaenda mahali mlango ulikuwa wazi huko juu, mahali palipokuwa na nuru, akaingia katika ubatizo wa Roho Mtakatifu katika chumba cha juu, huko juu ambako nuru ilishukia. Na bila shaka, kuna nuru zaidi kwenye orofa ya pili kuliko ingalikuwako kwenye—kwenye orofa ya kwanza. Na hivyo ndivyo ilivyokuja, daima.

⁷² Sasa, tunaona huko juu, ninawazia Nuhu alikuwa ameikusanya familia yake karibu na kusema, “Sasa, kutakapopambazuka asubuhi kutakuwa na giza kote angani, na mvua kubwa itakuwa ikinyesha, nao watu watajua basi ya kwamba nimetabiri yaliyo kweli.”

⁷³ Lakini unajua, baada ya kufuata kila agizo . . . Sasa, hapa ndipo ninapotaka muangalie: Ukiisha kufuata kila agizo, basi kama jambo fulani likitukia ambapo haliendi vizuri, wengi hukata tamaa, hiyo inaonyesha hawakuamini yale waliyokiri walikuwa wakisema. Mungu huwajaribu watoto Wake.

⁷⁴ Sasa, sikilizeni ujumbe. Nuhu, kwenye siku ya kumi na saba ya Februari, kulingana na Neno la Mungu, aliingia kwenye safina hiyo, na kesho yake asubuhi wote walikuwa huko wakitarajia kuona mvua ikianza kunyesha, bali jua lilichomoza

hasa kama lilivyofanya sikuzote. “Saa chache tu zaidi, nayo itaanza, mvua itaanza.”

⁷⁵ Hiyo siku ikapita, nami ningewazia moyo wa Nuhu ulianza kupepesuka. Ningeweza kusema jambo fulani papa hapa, lakini afadhali nisiseme. Lakini mnaona, asingeweza kutoka kama alitaka, alikuwa ametiwa muhuri ndani. “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu.” Mungu akaufunga mlango nyuma yake.

⁷⁶ Naye Nuhu akaketi pale, nao huo usiku ukapita, na siku kadhaa. Watazamaji wangekuja na kusema, “Vema, ninii. . . Loo, hakika, hao wanasayansi walikuwa sahihi, mzee huyo hakujua alichokuwa akizungumzia, si mvua. Na huyo hapo maskini jamaa huyo huko ndani amejifungia kwenye maskini mashua hiyo kubwa.”

⁷⁷ Loo, ni jambo kuu jinsi gani kufungiwa pamoja na Kristo! Hilo ni so—somo halisi. Basi mlango ukafungwa nyuma yake, asingeweza kuufungua, mkono wa Mungu tu ndio ungeweza kuufungua. Sasa, ndipo siku ya pili ikapita, na siku ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, mpaka juma zima likapita. Nuhu akaketi na kutoa jasho.

⁷⁸ Basi, tunapata somo gani kutokana na hilo? Kama Mungu. . . Vipi kama Bibi Shakarian angalisema. . .? Wakati Roho Mtakatifu aliponena, “BWANA ASEMA HIVI, kuna ukungu mweupe unaotoka kwake, huo ugonjwa wa mtoto wa jicho utatoweka,” wala haukutoweka kwa yapata majuma mawili au matatu, bali aliendelea kuketi pale akisema, “Haina budi kuwa hivyo. Haina budi kuwa hivyo.” Mungu hukuaacha utoe jasho wakati mwingine, lakini lazima ushikilie, ung’ang’anie, haidhuru unajisikiaje, kile unachowazia, ama chochote juu yake, shikilia tu. Kama kweli unaliadini, utashikilia, dumu moja kwa moja na imani yako. Mungu aliahidi jambo hilo, nawe ukajisikia umetiwa nanga moyoni mwako, kaa hapo.

⁷⁹ Ndipo kwenye siku ya mwisho ya juma, Nuhu akaamka asubuhi hiyo, nadhani mawingu yalikuwa yametanda kote. Wakaangalia nje kupitia dirisha la juu. Sasa, halikuwa pembeni mwa safina, Mungu hataki aangalie chini *huku*, anamtaaka aangalie *huko* juu, kwa hiyo lilikuwa juu ya safina. Naye alipoanza kuangalia, mawingu yalikuwa yanatanda juu, radi ilikuwa ikinguruma, nao watu wakaanza kukimbia kuelekea kwenye safina. Mitaa ikaanza kujaa matone makubwa ya maji, mifereji ya maji machafu yote ikajaa. Mbona, walidhani wangeweza kuyavuta kwa bomba, kama mafuriko yakija. Lakini mnaona, walitoa mashua, lakini kama haikuundwa na Mungu, ilizama; hakuna kitu kilichoilea ila hiyo safina.

⁸⁰ Na mnajua safina ilitengenezwa kwa mshita. Na kama ukiwahi kujua huo ulikuwa ni nini, ni mwepesi kuliko zeri. Si kitu. . . ni kama tu sifongo, mwepesi sana ungeweza kuchukua

boriti yake kubwa mno na kuinyanyua kwa mkono mmoja. Na si lingeonkana la ajabu kwamba Mungu angejenga safina Yake kwa kitu kama hicho? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kuimimina ndani ya huu upate kujaza vinyweleo, ndipo ukawa mgumu kuliko chuma.

⁸¹ Na hivyo ndivyo inavyotubidi kufanya, ni kuondoa kila kanuni ya imani, kila kitu kilicho ndani yetu, na kila upuuzi, na kila kutokuamini kuovu, ili Roho Mtakatifu apate kutujaza, na kutia muhuri kila kinyweleo cha kuamini kwetu, kila kinyweleo cha nia zetu, mpaka hutaona kama ni jirani yako, ama—ama ni nani anayeketi karibu nawe, umetiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu, ndipo unaweza kustahimili kupigwa na mawimbi unapopitia katika mateso.

⁸² Ndipo maji yakaanza kupanda juu ya kilima, nao watu wakaanza kupiga mayowe na kubisha mlango. Lakini Nuhu hata asingeweza kuwasikia, alikuwa ameketi huko juu kabisa juu ya jengo. Nao wakaangamia, kila kitu kilichopumua hewa juu ya nchi kiliangamia kwa . . . Na kitu kile kile kilichouua huo ulimwengu usioamini kilimwoko Nuhu.

⁸³ Hivyo ni kama vile ilivyo leo. Lile jiwe la kujikwaa, Roho Mtakatifu, anayeufanya ulimwengu mahali ambapo hawamtaki, Kitu kile kile wanachokikataa ndicho Kitu kile kile kitakacholipeleka juu Kanisa. Roho Mtakatifu atalitwaa Kanisa katika Unyakuo.

⁸⁴ Nuhu aling'ang'ania kwa sababu alijua Mungu alikuwa amesema naye. Haidhuru ilichukua muda gani, ama ni miaka mingapi, ama chochote kile, alishikilia kwa sababu alijua ilikuwa ni mpango wa Mungu.

⁸⁵ Musa, yule nabii mtoro, akiwa na dhana zote za kiakili ambazo mtu yeyote angeweza kuwa nazo, alikuwa mwerevu sana hata angeweza kuwafundisha Wamisri. Naye akajaribu kuongezea kwenye mpango wa Mungu kwa dhana yake ya kiakili, wala haikufanikiwa.

⁸⁶ Wala haitafanikiwa siku hizi. Hiyo ni kweli. Tunaliendea kwa njia mbaya, kanisa kwa jumla. Tunajaribu kuandaa namna fulani ya mpango.

⁸⁷ Unasikia u—uamsho unafifia, umefifia kabisa. Kuna shida gani? Ni kwa sababu tumeingiza mipango ye—yetu ya kujibunia ndani yake. Yote wanayohusika nayo leo ni, inaonekana kana kwamba, ni kujiunga na kanisa, kuwaingiza washiriki wapya, kujenga jengo kubwa, kudhamini kipindi fulani cha redio, ama kitu kama hicho.

⁸⁸ Tumepoteza shauku hiyo, kwa kweli, ya nafsi, utungu ule wa nafsi ambao Mkristo anapaswa kuwa nao, inaonekana tunaupoteza. Sizungumzi juu ya Wakristo halisi, ninazungumza juu ya wengi sana wanaokiri kuwa Wakristo.

⁸⁹ Sasa, yote unayosikia siku hizi ni kitu fulani kikubwa, na watu wakiingia katika matumizi ya mamilioni na...ya dola kwa mambo makuu. Na kisha ati kuhubiri ya kwamba Bwana yuaja katika kizazi hiki? Mbona, mwe—mwenye dhambi mtaani anajua huamini hilo, ama, matendo ya—ya—yako yananena kwa sauti kubwa kuliko maneno yako unapo—unapofanya hivyo. Bila shaka.

⁹⁰ Tunapaswa kwenda nyumba hadi nyumba, mahali hadi mahali, tukihubiri, na kulia, na kusihi, na kushawishi, tukijaribu kuingiza kila mtu katika Ufalme wa Mungu tuwezaye, tukiwatuma wamishenari mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini, na kila kitu tuwezacho kuwafanya watu waokoke.

⁹¹ Sasa, tunaona siku hizi sana sana ni juu ya kukata kauli. Unasikia hilo wakati wote, “kukata kauli.” Ninataka...Kukata kauli ni maungamo, maungamo ni mawe. Inafaa nini ku—kulundika lundo la mawe, kama huna mchonga mawe pale anayeweza kuyachonga, kwa Upanga mkali wa Mungu ukatao kuwili, kuwa wana na binti za Mungu? Kuwaacha wazurure hapa na kila namna ya wanawake, wamevalia kama mnyama aliyechunwa ngozi, na kujiita Wakristo, nao watu wakiwaacha wafanye hivyo, halafu wanajiita watumishi wa Kristo, nalo kanisa likiwa katika hali ya kawaida ya uvuguvugu lililomo, “mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake,” na kuyaita maamuzi?

⁹² Tunahitaji mawe yaliyochongwa yakawa wana na binti za Mungu kwa...Inafaa nini kubingirisha mawe kama hutayakata? Hayana budi kukatwa na kuingizwa katika mpango wa Mungu kwa karama na miito, na kuwekwa ndani ya Kanisa jinsi yanavyopaswa kuwekwa, hayana budi.

⁹³ Nuhu...Musa katika mawazo yake ya kiakili alishindwa kama tu kanisa zima lilivyoshindwa siku hizi. Watu wanaendelea kuishi moja kwa moja, wanaingia, wanakiri, wanaandika jina lao kwenye... “Ni barua, ni barua. Leta barua yako kutoka *hapa* uipeleke *kule*.” Si barua, ni kuzaliwa. Zaliwa mara ya pili, ndipo basi wewe ni wa *Huko* juu.

⁹⁴ Angalieni, lakini Nuhu, akishikilia kadiri alivyokuwa... Alikuwa amemsikia Mungu. Basi siku moja nabii huyu mtoro, huko nyuma upande wa nyuma ya jangwa, kweli alikuja kwenye mchanga huo mtakatifu, ambapo kila mhudumu anapaswa kuja. Haidhuru ana digrii ngapi za udaktari, profesa wa chuo, ama chochote anachoweza kuwa, hana shughuli yoyote mimbarani mpaka kwanza ashikwe kwenye mchanga huo mtakatifu kati yake na Mungu pekee, kwamba ana ujuzi na Mungu ambapo hakuna mwanasayansi ulimwenguni angeweza kamwe kumwondolea mbali.

⁹⁵ Wanaweza kuchukua Neno hilo na kulikata kwa njia yoyote watakayo. Ibilisi hutumia Neno, alilithibitisha, anatumia Neno kukata mpango wake mwenyewe. Lakini wakati mtu amewahi kuwa huko nyuma kwenye huo mchanga mtakatifu, ambapo hakuna kitu ila wewe na Mungu pekee kinachoweza kusimama, wanasayansi wote ulimwenguni wasingeweza kukuondolea hilo, kwa sababu ulikuwepo, nawe ukakutana na Mungu, nawe unajua kilichotukia. Hakuna mtu . . .

⁹⁶ Yesu asingewaruhusu kuhubiri mpaka walipopanda kwenda Yerusalemu na walikuwa . . . kumpokea Roho Mtakatifu kabla hawajaanza kuhubiri tena, hilo ndilo tukio.

⁹⁷ Wakati Musa alipopata tukio hilo la kile kichaka kilichowaka moto, ati kushikilia? Mbona, kosa moja dogo, naye akakimbia kutoka Misri. Basi angalieni, nje ya mapenzi ya Mungu alishuka akaenda kule na kumwua mtu mmoja, naye akalaumiwa, halafu basi Mungu akashuka pamoja naye na kuliua taifa zima, na ilikuwa ni utukufu. Hiyo ilikuwa ndiyo tofauti.

⁹⁸ Sasa, Musa . . . Wakati mwingine unapokutana na Mungu inakufanya utende mambo ya kiajabu, kweli unafanya. Sasa, Musa alikuwa wakati mmoja, alipotoka kwenda kuwakomboa hao watoto, alikuwa kijana shujaa na mwenye nguvu, lakini tunaona wakati alipofikia umri wa yapata miaka themanini, masharubu yake yakining'inia chini kabisa, na labda kichwa chake chenye upara karibu kilitokeza malengenge, kwenye jua, na wakati yeye, kesho yake asubuhi, alipokuwa amekutana na Mungu katika kijiti hiki kilichowaka moto, tunamwona akiwa na Sipora ameketi kwa kutagaa juu ya nyumbu, akiwa na mtoto wake nyongani mwake, akimwongoza punda huyu akiwa na fimbo iliopinda mkononi mwake, masharubu yakipepea, macho yake yametulia, akicheka tu na kumsifu Mungu.

Mtu fulani akasema, “Unaenda wapi, Musa?”

“Ninashuka kwenda Misri kuiteka.”

⁹⁹ Ilikuwa ni kitu gani? Uvamizi wa mtu mmoja. Lakini nini? Alishikilia kwa sababu alikuwa amekutana na Mungu, naye alijua Mungu alisema, “Hakika nitakuwa pamoja nawe.” Naye akafanya hivyo, akaiteka. Kwa nini? Angeweza kushikilia kwa sababu Mungu alisema, “Nitakuwa pamoja nawe.” Haileti tofauti yoyote yale kizuizi . . .

¹⁰⁰ Alipofika kule, jambo la kwanza alilokutana nalo lilikuwa mtu fulani aliyeweza kujaribu kuiga kazi aliyokuwa akimfanyia Mungu, jambo lile lile. Hivyo ndivyo ninyi daima, ninyi . . . kama nilivyosema, hivi majuzi usiku hapa, ama mkutano mwingine, sikuzote unakutana na matabaka matatu, ambayo ni waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini, na kwa hiyo, unawapata kila mahali.

¹⁰¹ Kwa hiyo hawa hapa wachawi wakaja kujaribu kuiga kwa utambuzi wa fahamu za juu sana, nao wakawatupa chini hawa nyoka kujaribu kuninii, ama, vijiti kuwafanya nyoka. Musa alikuwa amefanya yote aliyoweza kufanya, hivyo ndivyo Mungu alivyomwagiza kufanya, kwa hiyo akasimama tu kimya. Haleluya! Ukiisha kufanya yote uwezayo kufanya, basi ni juu ya Mungu kufanya yaliyosalia. Ndipo nyoka wa Musa akaja akawala wao.

Sasa, ninyi mnaoamini katika utambuzi wa fahamu za juu sana, ilikuwaje kwa hizo fimbo? Amina. Jambo ndilo hilo. Alishikilia.

¹⁰² Maskini Daudi siku moja, aliye mdogo sana na asiye na maana sana amesimama pale (Sauli, jemadari, tangu kichwa na mabega juu ya jeshi lake lote, jamaa mkubwa mno.), alimsahi Goliathi, ama, alikabili changamoto yake, hasa. Vema, sasa, Daudi, maskini jamaa mwekundu, mdogo, mabega yaliyoinama, amevaa fu—fulana ndogo ya ngozi ya kondoo hapa, alikuwa na kombeo, lakini alishikilia kwamba angeweza kupigana na jitu hilo. Ni kitu gani kilichompa ujasiri maskini jamaa huyo? Alikuwa na Kitu fulani ndani yake.

¹⁰³ Nilikuwa nikishuka kwenda, ninaamini ilikuwa ni Georgia, mahali fulani huko chini, nilikuwa, pamoja na Rufus Mosely na hao wengine, wengi wenu mlimjua, nami nilikuwa na m—mkutano huko chini katika uwanja wa kandanda, ndipo nikaona bango dogo ambalo daima lilinitia moyo, lilisema, “Si ukubwa wa mbwa katika pambano, bali ni ukubwa wa pambano katika huyo mbwa.” Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. Si lazima uwe na Ph.D., L.L., L.D. maradufu, Q.S.T., chochote kile, kitu pekee unachopaswa kuwa nacho ni maskini ujasiri mzuri wa Kikristo, pamoja na ufahamu ya kwamba Mungu alikutuma.

¹⁰⁴ Kama nilivyokuwa nikisema asubuhi ya leo juu ya Hudson Taylor, wakati mtu fulani alipomwambia, mvulana mdogo wa Kichina aliposema, “Bw. Taylor, ndiyo kwanza nimpokee Kristo. Inawaka moyoni mwangu. Sasa, itanibidi kuchukua miaka minne kupata B.A. ya—yangu, na digrii yangu ya udaktari, na kadhalika.”

Bw. Taylor akasema, “Usingoje mpaka mshumaa umeungua nusu kabla hujajaribu kuonyesha nuru yako,” kasema, “nenda ukafanye hivyo sasa.”

¹⁰⁵ Nikawaza, “Amina. Hiyo ni kweli.” Usingojee karibu na *hili*, *lile*, ama *linginelo*. Shule kubwa mno za theolojia, ziko sawa, zilikuwa katika siku zilizopita. Lakini, ndugu, tunachohitaji leo hii si shule ya theolojia, tunahitaji mishumaa iliyowashwa.

¹⁰⁶ Sikilizeni, endapo hujui zaidi juu yake, nenda ukawaambie jinsi ulivyowashwa, acha wawashe kutoka kwenye huo, na mtu mwingine akawashe nuru kidogo kutoka kwenye huo, tutakuwa na kurudi kwingine kwa Pentekoste. Kweli. Mara tu

unapowashwa, kama hayo tu ndiyo yote unayojua kuuhusu, nenda kamwambie mtu mwingine jinsi ulivyowashwa. Wakati mwingine makaburi haya, ama, seminari zinachukua yote, samahani, zinaondoa Nuru yote ndani yako. Hiyo ni kweli.

¹⁰⁷ Sasa, unang'ang'ania, waambie tu jinsi ulivyowashwa, useme, "Nilikuwa nimesimama pale, ndipo mara Roho Mtakatifu akanishukia. Kama utafanya jambo lile lile, itatendeka kwako." Sema kiasi hicho, kama hayo ndiyo tu ujuayo, simulia tu hayo, hayo yanatosha.

¹⁰⁸ Daudi, alijua ya kwamba Mungu alikuwa amemsaidia kwa kombeo hilo kuuu si—simba na dubu, naye aliona hali hiyo. Pia, Bwana alikuwa akinena moyoni mwake ya kwamba angempa ushindi dhidi ya jitu hilo, kwa hiyo akashikilia. Ndugu yake akasema, "Ninajua wewe ni mtukutu. Rudi kule ukawachunge hao kondoo." Lakini Mungu alikuwa na agizo, naye Daudi alishikilia mpaka akamwua Goliathi.

¹⁰⁹ Samsoni, bila kitu ila mfupa wa taya la nyumbu. . . Na hivi uliwahi kuchunguza jinsi silaha hizo zilivyokuwa kubwa kwa hao Wafilisti? Vema, ile chapeo iliyopita juu ya vichwa vyao, ikashuka juu ya masikio yao, ambapo wangeweza kuangusha mweko wa upanga wenye makali kuwili, unene wa shaba ulikuwa yapata inchi moja, ama inchi moja na nusu, chini juu ya vichwa vyao.

¹¹⁰ Nanyi mnajua jinsi maskini mfupa wa taya la nyumbu uliooza ungekuwa. Pigo la kwanza juu ya fuvu la kichwa, mbona, moja ya hizo chapeo lingepasua maskini mfupa huo wa taya vipande-vipande. Bali Daudi angeweza kugusa, na kuhisi hivyo vishungi saba, hivyo tu ndivyo alivyopaswa kuhisi. Ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yake, naye akawabwaga chini elfu moja wa hao Wafilisti kwa mfupa huo wa taya. Alishikilia, kwa sababu alijua ya kwamba hivyo vishungi saba viliwakilisha agano, naye Mungu alikuwa pamoja naye. Angeweza kung'ang'ania. Naam, bwana.

¹¹¹ Yohana Mbatizaji, hatuna habari nyingi juu yake. Tunajua baba yake alikuwa ni kuhani, nao walikuwa wakongwe, wote wawili, Elisabeti na—na Zakaria walikuwa na umri mkubwa. Hapana shaka kidogo ilikuwa ni vigumu kwa hi—hiyo familia, kwa sababu walijua hawangeishi kumwona mwana wao akiingia katika huduma yake, bali walijua hiyo ahadi ilitoka kwa Mungu. Walikufa, tunaambiwa.

¹¹² Badala ya Yohana kwenda, kama baba yake alivyofanya, kurudi kwenye chuo kile kile na shule ile ile, na kupata Ph.D., na kadhalika, na kujifunza, alikuwa na kazi ya kufanya, si kubusu watoto wachanga, na kuwaoza vijana, kuwazika wafu, ilimbidi kushika Upanga wenye ukali kuwili na kuwa kwenye mstari wa mbele wa vita, wala asingeweza kuchukua ujuzi wowote wa seminari, asingeweza kungojea hayo yote, kujifunza yote

jinsi ya kugeuzageuza kanuni zote za imani. Kama hayo ndiyo angalijifunza, hayo tu ndiyo angaliweza kuwapa watu.

¹¹³ Lakini alienda huko nje nyikani na kukaa, kwa sababu alikuwa amtambulisha Masihi, kwa hiyo akakaa huko mpaka Mungu akamwambia kile Masihi huyo angekuwa. Na kama Yohana alitaka, uh, alifanya hivyo, ni zaidi sana vipi sisi tunavyopaswa kuchunguza na kuona kile Roho Mtakatifu anachopaswa kufanya katika siku hii atakapokuja! Atatendaje? Itakuwaje?

¹¹⁴ Leo, wakati tumechanganyikiwa na kila namna ya mafundisho ya sharti, na mafundisho, na kudungwa sindano, na dawa ya kuhifadhi maiti, na kadhalika, halafu tunafanya hivyo wala hatuchunguzi, unalichukua tu kwa kudhania. *Kudhania* ni “kudiriki bila mamlaka halisi.” Usimdhania Mungu, amini Neno Lake na usonge mbele. Mungu anao mpango uliowekwa hapa, Yeye alitutabiria kwa manabii Wake kile ambacho kingetukia katika siku hii.

¹¹⁵ Yohana alikaa huko nje mpaka Mungu alipomwambia, “Sasa. . .” Sasa, bila shaka, wakati angalitoka nje na kusema, “Mimi ndimi mtangulizi, mimi ndimi niliyenenwa na nabii Isaya, mimi ndimi sauti ya mtu aliaye nyikani,” na sasa, hapana shaka ila ninii. . . mzee fulani wa wilaya, ama Kayafa fulani, ama askofu, ama mtu fulani alipitia hapo, akasema, “Unajua, Askofu Jones huko, daima nimewazia tu Yeye angekuwa Masihi. Kwa hiyo unajua, nina hakika tu. . .”

¹¹⁶ Hilo ni kosa lile lile ambalo Kanisa lilifanya kwa funguo Zake mpya. Yesu alimpa Petro funguo za Kanisa, alikuwa na funguo. Lakini walifanya nini mara ya kwanza walipozitumia? Walimchagua Mathiya kuchukua mahali pa Yuda, nalo halikufaulu, kamwe hakuna kitu kilichosemwa juu yake. Lakini Mungu alimchagua maskini Myahudi mdogo, mwenye hasira kali, mwenye pua iliyopinda, mwenye hasira kali, Naye akasema, “Nitamfanya upya, na kuonyesha yatakayompata kwa ajili Yangu.”

¹¹⁷ Ni Mungu anayepaswa kufanya mambo, si mwanadamu. Kwa hiyo tunaona ya kwamba Yohana hangeweza kumudu kwenda kule na kudungwa sindano ya kitheolojia ya seminari. Kwa hiyo jambo alilofanya ni kungojea huko, ndipo Mungu akamwambia, “Utakapoenda huko nje sasa, utakuwa na *hili, lile*, ama *linginelo*, lakini usilijali, Masihi huyo atakuwa na ishara ya Masihi, nawe utaiona. Itakuwa ni Roho ya . . . atashuka kutoka Mbinguni kama hua, na atashuka juu Yake, basi huyo ndiye Masihi.”

¹¹⁸ Naye Yohana alishikilia sana kwamba atakuja katika kizazi chake, kamwe hakujenga shule zozote kubwa, kamwe hakuwa na seminari kubwa na kuwakaribisha watu humo. Alifanya nini? Alikuwa na hakika sana, hata akasema, “Kuna Mtu aliyesimama

miongoni mwenu sasa,” amina, “hamumjui, lakini Yeye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu. Ninajua Yeye yupo hapa.”

¹¹⁹ Haleluya! Jinsi tunavyoweza kusema jambo lilo hilo usiku wa leo! Kwa ishara za Roho Mtakatifu, tunajua Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste yupo hapa, Kitu kile kile. Jambo lile lile ambalo Mungu alisema angefanya katika siku hizi za mwisho.

Samahani kwa kutokukaa hapa nyuma, lakini kama mlijisikia kama nilivyojisikia, mngetembea pia.

¹²⁰ Kwa hiyo, wao. . . Yohana alikuwa na hakika, naye alijua ishara hiyo ya Masihi ingekuwa nini, kwa hiyo ye—yeye alishikilia kabisa kwamba angemjua. Siku moja Yeye alikuja akitembea miongoni mwao, akasema, “Tazameni Mwana-Kondoo wa Mungu, aondoaye dhambi ya ulimwengu.” Akasema, “Yeye aliyeniambia, huko nyikani, kubatiza kwa maji, alisema, ‘Ambaye utamwona Roho akishuka, na kukaa juu Yake, Huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.’”

¹²¹ Sasa, safari ndefu kulifikia somo langu. Lakini maskini mwanamke huyu tunayesoma habari zake, alikuwa ni Myunani, bali alikuwa amesikia habari za Yesu. Nayo imani chanzo chake ni nini? Kusikia, kusikia Neno la Mungu. Sasa, yeye alikuwa Myunani, wa taifa lingine. Sasa, lakini mnajua, ingawa hakuwa katika imani ya jambo hilo, alikuwa wa jamii tofauti ya watu, hata hivyo, mwajua, imani hupata Chanzo ambacho wengine hawakioni. Imani hupata Chanzo ambacho wengine hawakioni, nayo imani yake ilikuwa imekipata Chanzo hicho. Sasa, yeye alijua ya kwamba, kwa kusikia, kama angefika kule, yale yaliyokuwa yanaenda kutukia.

¹²² “Neno la Mungu,” kulingana na Waebrania, mlango wa 4 na kifungu cha 12, “ni kali kuliko upanga ukatao kuwili.” Tunajua hilo, na imani ndiyo inayoshikilia upanga huo. Hakuna kitu kingine kinachoweza kushikilia upanga wa Biblia ila imani katika Mungu, hiyo inautumia. Sasa, huenda ukawa dhaifu kwa mkono wako wa imani, labda unaweza tu kukata kuhesabiwa haki, labda unaweza tu kukata vya kutosha kujiunga na kanisa. Lakini mkono mzuri, wenye nguvu wa imani unaweza kukata ukaingia kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu, unaweza kukata ukaingia kwenye uponyaji wa Kiungu, unaweza kukata ukaingia kwenye karama, miujiza, ishara, maajabu, unaweza kukata kila ahadi ya Mungu kutoka mbinguni na kuidai, kwa sababu inalitumia Neno la Mungu.

¹²³ Alikuwa na vizuizi vingi, kama ungeanza kuwazia juu yake, bali imani yake haikuwa na chochote. Jambo ndilo hilo. Kama imani yako haina vipingamizi vyovyote, ni tofauti. Alikuwa nayo, bali imani yake haikuwa na vizuizi. Imani haijui kizuizi chochote, imani inajua tu jambo moja, lengo lake, hivyo tu.

124 Huenda mtu fulani alimwambia, “Sasa, ngoja kidogo, wewe ni Myunani, huna shughuli.” “Wewe ni Mmethodisti, hupaswi kwenda kwa hao Wapentekoste.” “Wewe ni Mbaptisti, hupaswi kwenda kule. Unaona?” Lakini hilo halikumzuia, alikuwa ameshikilia. Alikuwa ameng'ang'ania sana.

125 Na huenda kulikuwa na kundi lingine lililomjia na kusema, “Sasa, ngoja kidogo hapa, kipenzi. Unajua nini? Siku za miujiza zimepita.” Lakini hilo halikumkomesha. Kwa nini? Imani ilikuwa imeshikilia, naye alikuwa angali ameshikilia, alikuwa akienda haidhuru.

126 Halafu kuna kundi lingine. Baadhi ya wanawake wa kanisa lake huenda walikuja huko, na kusema, “Mpenzi, unajua nini? Ukienda *kule*, mumeo ni shemasi *hapa*, atakuacha, hivyo tu. Kutakuwako na talaka katika familia yako.”

127 Lakini imani ilikuwa imeshika Kitu fulani, Neno la Mungu, naye akaondoka kwa vyovyote vile. Aling'ang'ania, hangechukua “La” kama jibu, imani ilikuwa imeshika Kitu fulani. Laiti ingefanya hivyo usiku wa leo, kila mtu hapa, imani ishikilie. Haijui chochote ila ukweli, hivyo tu.

128 Sasa, vema, huenda kulikuwa na kundi lingine lililojitokeza, likasema, “Utachekwa, utaitwa ‘mtakatifu anayejibingirisha.’ Kama ukiwahi kwenda kule utahesabiwa kuwa ni mmoja wao.” Lakini mnajua nini? Bado alishikilia, alikuwa akienda, haidhuru alitwaje, imani ilikuwa imeshikilia.

129 Sasa, hapo, huenda hapa kundi la wahubiri wa imani yake mwenyewe lilimjia, na kusema, “Unajua,” ama—ama, imani ambayo watu wake walikuwa nayo, na wangesema, “unajua nini? Ukienda, utafukuzwa kanisani mwako.” Lakini bado alikuwa ameshikilia. Alikuwa anaenda kufika huko kwa vyovyote vile, haidhuru mtu yeyote alisema nini, alitaka kufika huko.

130 Hatimaye akawasili. Kama vile Nuhu, akawasili. Lakini alipofika kwa Yesu, alifikiri yote yalikuwa yamekwisha basi. Na mara nyingi watu hufikiri kwa sababu Mungu anakubariki, anawapa mkutano mzuri, ama anakupa msisimko mkubwa wa imani upesi sana, Bwana anenee nawe, na kukuita ukiwa mkutanoni, unawazia, “Loo, ndivyo hivyo tu.” Lakini kumbukeni, kuna kuvunjika moyo hapo pia, Mungu humjaribu kila mtoto amjiaye, kila mwana.

131 Kwa hiyo alipofika kwa Yesu, alifikiri yote yamekwisha, mwajua, alipofika kwa Yesu, lakini upesi akageuka, kwa kuvunjika moyo sana, na kusema, “Sijatumwa kwa jamii yako.” Sasa, baada ya kulazimika kupitia kila moja ya hivi vizuizi, naye alikuwa ameviruka kila kimoja kwa imani yake, kisha akamfikia huyu Yesu wa Nazareti, basi mara alipofika pale na kuanza kumlilia, Yeye alimpuuza, akaondoka, kisha hatimaye

akageuka kwa kukemea na kusema, “Sijatumwa kwa jamii yako. Nimetumwa tu kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.”

¹³² Ni kemeo jinsi gani! Kama huyo angalikuwa ni baadhi ya watu wetu wa Kipentekoste, wangalisema, “Vema, kama hivyo ndivyo anavyojisikia kulihusu!” Halafu basi, isitoshe, akasema... alitambua... Naye akasema, jambo lingine, Yeye alisema jamii yake ilikuwa ni kundi la mbwa. Loo, jamani, ujasiri wenyewe! Hilo si lingetikisa Mpentekoste?

¹³³ “Mungu abarikiwe, nitaenda kwa Assemblies sasa, ama huko kwa Church of God, ama Foursquare. Kama huninii... nitaliacha kundi lote na kuwaendea Wabaptisti. Wasiponikubali, nitaenda kwa Presbiteri. Hatimaye nitaishia kuwa Mkatoliki, nadhani.” Mnaona? “Loo, hakika, hawataniita kitu kama hicho, kusema mimi ni mbwa. La.”

¹³⁴ Naam, alimwita mbwa, kasema, “Sijatumwa kwa jamii ya watu wenu, nimetumwa tu kwa Wayahudi. Sijatumwa kwenu, na isitoshe, watu wenu ni kundi la mbwa tu.” Hmm! Lakini bado alishikilia. Loo, jamani! Ninapenda hilo. Sasa, ninajisikia kubarikiwa. Amina.

¹³⁵ Ninapenda hilo. Haidhuru kizuizi kilikuwa nini, bado alishikilia imani hiyo. Hapo ndipo unapolipata, ndugu. Amina. Yote, kila kitu ulimwenguni kisingeweza kukuondoa kwake. Hiyo ni kweli.

¹³⁶ Alishikilia, haidhuru mtu mwingine yeyote alisema nini, alishikilia, hata Yesu Mwenyewe alisema, “Sijatumwa kwa jamii yenu, nanyi ni kundi la mbwa. Wala sitachukua chakula cha watoto na kuwatupia ninyi mbwa.” Loo, jamani! Lakini bado alishikilia. Ninapenda hilo.

¹³⁷ Yeye hakuwa mmea wa tuta, namna fulani ya chotara kama mazao ya kisasa yalivyo siku hizi. Nilisema nini basi? Angalieni, hiyo ni kweli, mmea wa tuta hauna budi kubembelezwa, inakubidi kumnyunyizia wakati wote, kumpigapiga begani, bali mmea wa kale ulio imara uliotokea huko nje kwa nguvu za asili, huhitaji kumnyunyizia, wala hakuna mdudu atakayemsumbua. Amina.

¹³⁸ Ni kitu hiki chotara, inakubidi kuwapigapiga begani. Endapo Wamethodisti hawawataki, Wabaptisti watawachukua. Kama *hili* haliwataki, *hilo* lingine litawachukua, hiyo ndiyo sababu hawana imani. Hakuwa mmoja wa hao machotara, la, bwana, mmea wa tuta. Alijua alichokuwa akitafuta, naye alikuwa ameshika kitu fulani kilichokuwa kinaenda kumpa hicho. Amina. Amina. Ninapenda hilo. Naam, bwana. Hakuwa zao la kisasa tu—tulilo nalo siku hizi. Alidumu nacho.

¹³⁹ Angalieni, yeye pia alikubali ya kwamba aliyosema Yesu yalikuwa ni kweli. Whiu! Jamani! “Mimi ni mbwa.” Amina. Imani, sikilizeni, Yesu alikuwa ni Neno, na kama una imani halisi, imani daima itakubali kwamba Neno ni kweli. Imani

kamwe haitabishana dhidi ya Neno, amina, itadumu na Neno. Jinsi Neno lilivyosema ufanye, hivyo ndivyo imani itakavyolitambua. Nitaacha tu hilo lizame kwa dakika moja. Naam, imani hukubali ukweli.

¹⁴⁰ Akasema, “Ni kweli.” Alikubali Yeye alikuwa sahihi, imani daima itafanya hivyo. Mnaona, alikuwa ameshika kitu cha juu kuliko. . . kizazi hicho chote cha Kiyahudi kilichoshikilia wakati huo. Alikuwa na kitu alichokuwa amekishikilia ambacho kilikuwa. . . kisingeachilia. Kulikuwa na kitu fulani ndani, kilichodundadunda ndani yake hata alijua angejibiwa ombi lake. Haidhuru kama aliitwa “mbwa,” ataitwa chochote, atupwe nje, akanyagwe, chochote kile, alikuwa ameshikilia kitu fulani ambacho alijua kilikuwa kinaenda kumtimizia haja yake.

¹⁴¹ Mungu akirehemu kizazi hiki cha watu wenye dhambi. Shikilia. Kama hilo ni Neno la Mungu, kila Neno Lake ni kweli. Ishi Kwalo, ufe Kwalo. Nayo imani ya Roho Mtakatifu itaitikia kila ahadi kwa “Amina.” Hiyo ni kweli.

¹⁴² Aliishikilia, akasema, “Ni kweli, Bwana, mimi sistahili. Mimi ni Myunani, mimi si wa watu Wako, nami ni mbwa. Wala sisi ukanibembeleze, na ikubidi kuniwekea mikono, na. . .”

Kama vile Naamani ama baadhi yao, “Hakika angekuja, akaweka mikono yake juu yangu, akauondoa ukoma.”

Nabii alisema, “Nenda ukajitumbukize katika Yordani.” Loo, jamani!

¹⁴³ Mnaona, hiyo ndiyo sababu watu wanalikosa, wanataka kulipata jinsi wanavyotaka. Mungu hulitoa jinsi anavyotaka kulitoa. Tunataka. . . tuna njia moja iliyowekwa, hatuna budi kupitia njia hiyo. Hivyo tu. Lakini Mungu hulifanya kwa njia Yake.

¹⁴⁴ Akasema, “Ni kweli, Bwana. Mimi sistahili, nami ni mbwa, ndiyo kwanza Wewe uniite mbwa. Lakini mbwa hula makombo yanayoanguka kutoka mezani pa bwana wao.” Jambo ndilo hilo! Alikuwa tayari kula makombo.

¹⁴⁵ Ni tofauti jinsi gani na sisi Wapentekoste! Mnajua sisi Wapentekoste tuna shida gani? Tumeona mengi sana, hata yamekuwa ya kawaida kwetu, tumebarikiwa sana. Hiyo ndiyo shida yetu sisi Wamarekani.

¹⁴⁶ Ninapoenda India, na kuwaona hao watoto wachanga wamelala kule, na maskini matumbo yao yamevimba kwa njaa, naye mama amelala barabarani akifa, katika sehemu kama hizo, na kuona njaa na ukosefu wa chakula, naja huku, na kuona cha kutosha kimezolewa kwenye mapipa ya takataka kinachoweza kuwalisha, nawaona wanawake hawa wakitoka, na kulipa dola nane kwa ajili ya chakula cha mchana alasiri, kitu kama hicho, na kukinyofoa kwa dakika chache na kuzungumzia shirika la namna fulani, kisha wanakitupa kwenye pipa la takataka,

ambacho kingewalisha baadhi ya watoto wa Korea wenye njaa! Halafu tunajiita taifa la Kikristo. Tunalishwa vizuri.

¹⁴⁷ Wapentekoste wanazunguka, kisha wanarudi, na wanapitia hayo, na kuona mkutano kama wa Oral Roberts, yale Mungu anayofanya na Oral, wanarudi, na kuona huyu *mwingine*, na huyu *mwingine*, na huyu *mwingine*, yote Mungu akifanya kazi, ndipo muda si muda mwajua, wanaketi tu kitako, na kulichukulia tu kwamba ni la kawaida.

¹⁴⁸ Kama vile maskini baharia wakati mmoja, akitoka baharini, ndipo akakutana na mshairi, mshairi Mwingereza. Naye akamwambia huyo mshairi, huyo mshairi alikuwa ameandika mashairi mengi kuhusu bahari, ndipo yule baharia mzee akasema, “Unaenda wapi, mtu wangu mwema?”

¹⁴⁹ Akasema, “Loo, ninaenda baharini. Sijawahi kuona, hata hivyo nimeandika habari zake kutokana na yale niliyojifunza kwenye vitabu,” akasema, “lakini kwa kweli sijawahi kuona bahari. Ninatamani kunusa harufu ya mawimbi ya bahari ya chumvi, Ninapenda kuona anga la samawati likiakisi katika maji yake ya samawati, ninatamani kusikia mlio wa shakwe wa baharini.”

¹⁵⁰ Yule baharia mzee, huku amesimama pale na kiko kikubwa kinywani mwake, akatema mate, na kusema, “Vema, nimeishi juu yake kwa miaka hamsini, wala sioni kitu cha kulisimua sana kwake.”

¹⁵¹ Kwa nini? Alikuwa ameiona sana mpaka akawa, ikawa ni kawaida kwake. Na hivyo ndivyo watu, wanavyoona katika siku hizi za mwisho, wakati Biblia inaponea yale hasa Roho Mtakatifu, na yale Kristo atakayofanya kwenye kule kuonekana kabla tu ya kule Kuja, nao wanaona hilo jambo likitukia, na kusema, “Vema, vizuri sana, nadhani hilo ni sawa.” Loo, jamani! Linapaswa kuitikisa mioyo yetu, linapaswa kutufanya tushikilie kujaribu kuupeleka Ujumbe kwa watu kabla haijachelewa sana.

¹⁵² “Bwana, ninataka tu makombo.” Kumbukeni, kamwe hakuwa ameona mwujiza, alikuwa ni Myunani, bali alikuwa amesikia kwamba kulikuwa na mwujiza, kwamba Yesu alifanya miujiza. Naye alijua kama Yeye angeweza kufanya miujiza kwa ajili ya mtu mmoja, Mungu alikuwa Muumba wa vitu vyote, na watu wote, Naye angeweza kuifanya kwa ajili yake. Hakuwahi kuona mwujiza, bali hata hivyo alikuwa akiamini apate mmoja, nasi tunaiona siku baada ya siku na usiku baada ya usiku, hakuwa amewahi kuuona.

¹⁵³ Alikuwa kama yule kahaba Rahabu wakati wale wapelelezi walipokuja, kamwe hakusema, “Sasa, ngojeni kidogo, hebu niende nikamwone Yoshua, hebu nione jinsi anavyovalia nguo zake, hebu nione jinsi anavyochana nywele zake, hebu nimwone akifanya miujiza.” Kamwe hakuomba hilo, la. Hiyo ndiyo sababu alihesabiwa haki, kwa sababu aliikubali kwa imani.

154 Akasema, “Nimesikia!” Amina. “Ninataka Mungu huyo awe Mungu wangu.” Akasikia. Na aliposikia, ilikuwa ni Mungu akitenda kazi. Naye alijua ilikuwa ni Mungu, kwa sababu alikuwa ameona ishara ya Mungu ambaye angeweza kushinda mamlaka yote ya wafalme ulimwenguni. Alikuwa tayari kulipokea. Naam.

155 Loo, jamani! Angalieni kile hilo lilichomfanyia Yesu, Yeye alisema, “Kwa msemu huu...” Kwa msemu huu... Mnaona, alikuwa na mtazamo mzuri kwa karama ya Mungu, huna budi kuliendea vizuri. Unapoketi huko nje, unapokuwa kanisani, unapokuwa madhabahuni, popote ulipo, huna budi kumwendea Mungu kwa njia ifaayo. Upendeleo... Imani daima huikubali kweli.

156 Martha, hebu tuzungumze habari zake kwa dakika chache tu. Martha, daima tunafikiri alikuwa mzembe sana, kuhusu kuisafisha nyumba yake wakati alipokuwa akienda kumkaribisha Yesu. Mariamu, mzembe kidogo upande wake, aliketi tu hapo, akasikiliza. Yesu, bila shaka, alisema alisikiliza mambo yaliyo bora zaidi. Lakini Martha alionyesha kile alichokuwa, kile kilichokuwa moyoni mwake, alijua ya kwamba Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu.

157 Hapana shaka alikuwa amesoma hadithi nyingi za Biblia. Alikuwa amesoma kuhusu yule mwanamke Mshunani, na jinsi huyo mwanamke alivyokuwa amepita umri wa kuzaa, naye alikuwa amemtengenezea nabii chumba kidogo, kwa sababu alimwambia mumewe, “Ninaona ya kwamba huyo ni mtu mtakatifu anayepitia njiani mwetu. Nakuomba, tafadhali, na tufanye chumba kidogo kando ya nyumba yetu, apate kupumzika. Na kama hatuko nyumbani, anaweza tu kuingia, anaweza kuwa na ufunguo mlangoni.” Naye alikuwa akionyesha wema.

158 Ndipo Eliya akampa baraka, na kumwambia atapata mwana. Wakati mwana huyo aliposhikwa na ugonjwa kwenye umri wa miaka kumi na miwili hivi, hapana shaka alishikwa na ugonjwa wa jua kali, akalia, “Kichwa changu, kichwa changu,” baba yake alikuwa amemwingiza ndani, ama, aliagiza aingizwe ndani, akamweka pajani mwa mama yake mpaka adhuhuri, kisha akafa.

159 Sasa, angalieni imani ya mwanamke huyo, alimchukua na kumlaza kwenye kitanda cha nabii. Um-hum! Ni mahali pa jinsi gani pa kumweka! Mnaona? Akamlaza kwenye kitanda kile, naye akasema, “Tandika nyumbu sasa, wala usisimame mpaka nitakapokwambia usimame.” Na kwa hiyo akaondoka kwenda mlimani ambako, alienda kwenye pango hili, alipokuwa Eliya.

160 Mungu hawaambii manabii Wake kila kitu, kile tu anachotaka wajue. Ndipo Eliya akaangalia juu, akamwambia Gehazi, kasema, “Huyu hapa yule Mshunani anakuja. Nami...

Amejaa huzuni, sijui ni nini, Mungu amenificha.” Akasema, “Hujambo? Mume wako hajambo? Mtoto hajambo?”

Mwangalieni yule mwanamke Mshunami, “Hatujambo.” Amina.

¹⁶¹ Ati nini? Alikuwa mbele za mtu, wakala wa Mungu, mtu ambaye angeweza kufanya mwujiza, ambaye angemchukua mwanamke wa umri wake, aliyepita umri wa kuzaa, na mzee kama mumewe, na kuwabariki katika Jina la—la Bwana Mungu, na kuona ono, na kumwambia angemkumbatia mtoto, naye akamkumbatia. Alijua basi huyo alikuwa ni mtu wa Mungu.

Kwa hiyo akasema, “Hebu niende kwake.” Naye alipofika kwake alisema, “Hatujambo.” Amina. Ninapenda hilo. “Yote ni sawa.” Ndipo akaanza kufunua.

¹⁶² Ndipo Eliya, akamwambia Gehazi, kasema, “Chukua fimbo hii,” maana Eliya alijua ya kwamba kila kitu alichogusa kilibarikiwa. Sasa, kama huyo mwanamke angeamini hilo ama la, sijui. Nafikiri hapo ndipo Paulo, akiwa wa kimsingi, alipopata wazo la kuweka lesa na nguo alizotoa mwilini mwake zikawekwa juu ya watu.

Ndipo Eliya akasema, “Chukua fimbo hii, jifunge viuno vyako, mtu yeyote akikuzungumzia, usimjibu, nawe uende, ukaiweke hii juu ya huyo mtoto aliyekufa.”

¹⁶³ Lakini imani ya huyo mwanamke haikuwa kwenye hiyo fimbo, ilikuwa katika huyo nabii. Fimbo haikumwambia hivyo, nabii alimwambia hivyo. Naye alishikilia, akasema, “Kama Bwana aishivyo, na nafsi yako haifi kamwe, sitakuacha.”

¹⁶⁴ Loo, napenda hilo. Mungu abarikiwe, laiti watu wangelimshika Roho Mtakatifu, Wakala wa Mungu duniani usiku wa leo, na kumshikilia namna hiyo, “Sitamwachilia.” Huenda ikakubidi kushindana mwereka kama Yakobo usiku kucha, bali utapata haja yako. Mshikilie, ng’anga’nia. Naye akashikilia mpaka akapata haja yake.

¹⁶⁵ Labda Martha alikuwa amesoma hadithi hiyo. Naye alijua kama Mungu alikuwa ndani ya nabii huyo, ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Mtu wa majira hayo, na hakika Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe kama alikuwa katika nabii Wake. Kwa hiyo anatoka kwenda kumlaki, na wakati alipokutana Naye, angaliweza kumkemea, sasa, kwa sababu aliagizia aje, Lazaro alikuwa amekufa siku nne naye alikuwa ananuka. Naye akatoka mbio kumlaki, alisikia Yeye alikuwa yuaja, kwa hiyo alishikilia, akaondoka kwenye msafara wa mazishi akaenda mbio kumlaki Yesu. Ingawa alikuwa tayari amemkatalia, alienda kumlaki; alishikilia.

¹⁶⁶ Ndipo akamwendea mbio, naye akasema, “Bwana, kama ungalikuwa hapo, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Ninapenda

hilo. Mnaona? “Ingawa amekufa, ingawa ananuka, hata hivyo lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

¹⁶⁷ Sasa, hiyo ndiyo njia ya kufanikisha jambo. Sasa, hivyo ndivyo ninyi kusanyiko mnavyopaswa kujisikia kuhusu mchungaji wenu. Mnaona? Hapo ndipo Mungu atakapojibu. Hiyo ni kweli. Huna budi kuziendea karama za Mungu kwa njia ifaayo, kwa uchaji. Na huduma ni, kutumikisha karama. Ni karama katika mwili, karama tano za kiroho ambazo, zilichaguliwa tangu zamani na kukusudiwa tangu zamani na Mungu kwa Kanisa. Ninajua kuna karama tisa za mahali hapo mwilini, lakini hizi ni karama za ofisi ya Mungu, ofisi, mitume, manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti. Nasi hatuna budi kuwaheshimu kama tunatarajia kitu kutoka kwa Mungu.

¹⁶⁸ Akamkimbilia moja kwa moja, naye akasema, “Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Ninapenda hilo.

¹⁶⁹ Ingawa daktari alisema *hivi*, “Lakini hata sasa, Bwana . . .” Daktari anasema una kansa, “Lakini hata sasa, Bwana . . .” Daktari anasema huwezi kupona, “Lakini hata sasa, Bwana . . .” Jambo ndilo hilo. “Hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu . . .” Naye ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu, “Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, anayeishi daima ili kutuombea.” Loo, jamani! Nguo Zangu Mwenyewe zilizojaa Damu zikiwa mbele ya madhabahu ya Mungu. “Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.”

¹⁷⁰ Imani yako inaweza kungusa Naye anaweza kuchukua ofisi Kanisani, na kujibu moja kwa moja kupitia midomo hiyo, na kuwaambia hasa. Atafanya kazi ile ile aliyofanya alipokuwa hapa duniani, aliahidi kuifanya, Naye anaifanya. Amina. Kwa nini hatuwezi kushikilia? bila shaka, tukiwa na kitu kama hicho, zaidi sana kuliko alichokuwa nacho.

¹⁷¹ Angalieni, sasa, naye Martha, alisema, “Hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Angalia jambo hilo, ingawa alikuwa amemkataa, kasema, “Jambo pekee ninalotaka ufanye ni kuomba tu maombi, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

¹⁷² Sikiliza jambo hili, jamani, magurudumu yanaanza kuungana basi, imani ikaanza kukutana na Mungu. Ni kama tu kuweka hasi na chanya pamoja, utapata nuru hivi karibuni sana.

Sasa, mnaona kilichotukia. Sasa, Yeye alisema, “Ndugu yako atafufuka tena.”

Akasema, “Naam, Bwana, atafufuka tena katika siku ya mwisho, ule ufufuo wa kيامa. Alikuwa mvulana mzuri, atatokea.”

¹⁷³ Ndipo Yesu akasimama wima. Mnaona, mambo ndiyo kwanza yaanze kutukia sasa, mwanamke alikuwa akitokwa na jasho, kama vile Nuhu, na kama mwanamke huyu tunayenena habari zake, huyu Myunani, akitokwa na jasho. Akasema, “Mimi ndimi Ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Je, unasadiki haya?”

¹⁷⁴ Akasema, “Naam, Bwana,” loo, jamani, “Ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu aliyekuwa aje duniani.” Haya basi. “Ninaamini ya kwamba Wewe ni kile unachokiri kuwa, Mwana wa Mungu.” Jambo fulani halina budi kutukia. “Ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu ajaye ulimwenguni.”

¹⁷⁵ Mwanamke fulani alikutana nami miaka kadhaa iliyopita naye alikuwa akijadili hilo nami, akaniambia, akasema, “Ndugu Branham, kuna kosa moja tu ninalopata katika kuhubiri kwako.”

Nami nikasema, “Asante! Kama ni kosa moja tu, hilo ni—hilo ni zuri sana.”

Naye akasema, “Hilo ni hili: unajivunia Yesu kupita kiasi.”

Nikasema, “Loo, jamani, kama ndivyo ilivyo! Ni—nina furaha sana kwamba ninafanya hivyo.” Nikasema, “Siwezi kujivunia vya kutosha.”

¹⁷⁶ Akasema, “Lakini unaona, Bw. Branham, hili hapa jambo moja. . .” Kanisa lake haliamini Yeye ni Mungu, linaamini tu Yeye alikuwa ni nabii. Kama Yeye alikuwa tu ni nabii, sote tumepotea. Kama Yeye ni kitu chochote pungufu ya Mungu, sote tumepotea, hiyo ni kweli, bila shaka. Alikuwa Mungu.

Naye akasema, “Unamfanya Mungu, naye hakuwa Mungu.”

Nikasema, “Yeye alikuwa ni Mungu.”

Akasema, “Unadai unaamini Biblia.”

Nikasema, “Naam.”

Naye akasema, “Kama nitathibitisha kwa Biblia yeye hakuwa Mungu, utakubali?”

Nikasema, “Kama Biblia ilisema Yeye hakuwa Mungu nitakubali, lakini huwezi kuthibitisha hilo.”

Akasema, “Nitalithibitisha.”

Nikasema, “Vema.”

¹⁷⁷ Akasema, “Katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 11, Biblia ilisema ya kwamba wakati Yesu alipoenda kwenye kaburi la Lazaro alilia, na kama alikuwa ni Mungu, asingeweza kulia.”

¹⁷⁸ Nikasema, “Mama, hoja yako ni nyembamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa.” Nikasema, “Hata hu—huna wazo hata kidogo. Naam,” nikasema,

“Yeye alikuwa ni Mungu,” nikasema, “Alikuwa Mungu na mwanadamu pia.” Kweli. Nikasema, “Yeye alikuwa mwanadamu wakati alipokuwa akilia, lakini aliposimama kando ya kaburi lile ambamo mtu aliyekufa alikuwa amekufa siku nne, na kusema, ‘Lazaro, simama kwa miguu yako,’ huyo hapo anarudi mtu aliyekuwa amekufa siku nne, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu.” Hakika alikuwa.

¹⁷⁹ Yeye alikuwa mwanadamu wakati alipotoka kilimani usiku huo, akiwa na njaa, akiangalia juu ya mti apate chakula, Yeye alikuwa mwanadamu wakati alipokuwa na njaa, lakini wakati alipoweza kuchukua biskuti tano na samaki wawili na kuwalisha elfu tano, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu, Muumba. Kweli.

¹⁸⁰ Alikuwa mwanadamu wakati alipolala nyuma ya chombo hicho usiku huo, nguvu zilikuwa zimemtoka, midomo Yake ilipasuka kutokana na kuhubiri, akapwelewa Sauti Yake, nzito. Alikuwa amelala usingizi kwenye meli hiyo, mpaka pepo elfu kumi wa baharini wakaapa wangemzamisha usiku huo, walipokuwa naye amelala pale kwenye mto nyuma ya mtumbwi, huku mawimbi yakipiga huku na huko hata hayangeweza kumwamsha. Alikuwa Mwanadamu wakati alipokuwa amelala, alikuwa mwanadamu wakati alipokuwa amechoka.

¹⁸¹ Lakini walipomwamsha, Naye akasimama huko nje, na kuweka mguu Wake kwenye demani ya hicho chombo, akaangalia juu, na kusema, “Amani, tulia,” nazo pepo na mawimbi yakamtii, huyo alikuwa...huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu, huyo alikuwa ni Mungu ndani ya mtu huyo, Yeye alikuwa ni Mungu. Alikuwa zaidi ya nabii, Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii, Mungu na mwanadamu pia, Yehova aliyefanyika mwili kuondoa uchungu wa mauti.

¹⁸² Angalia, Yeye alikuwa mwanadamu wakati alipolia apate rehema msalabani, hiyo ni kweli, lakini kwenye asubuhi ya Pasaka, wakati alipovunja mihuri ya mauti, kuzimu, na kaburi, na kufufuka tena, kasema, “Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa, na ni hai milele na milele,” huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu.

¹⁸³ Kila mtu ambaye amewahi kuwa na thamani yoyote ndogo katika dunia hii wamekuwa ni watu walioamini hilo, hata kwa washairi, mmoja alisema:

Alipoishi, alinipenda; akifa, Yeye aliniokoa;
Alipozikwa, alizipeleka dhambi zangu mbali sana;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
Siku moja Yeye yuaja—loo, siku tukufu!

Eddie Perronet, aliyeandika, akiteswa, aliandika wimbo wa uzinduzi wa Kuja Kwake, akasema:

Nyote zisifuni nguvu za Jina la Yesu!

Malaika na wasujudu;
 Leteni taji ya kifalme,
 Na kumvika taji Bwana wa wote;

Mungu aliyedhihirishwa katika mwili! Bila shaka.

Kipofu Fanny Crosby, unaweza kusema nini juu Yake?
 Alisema:

Usinipite, Ee Mwokozi Mpole,
 Sikia kilio changu kinyenyekevu;
 Unapowazuru wengine,
 Usinipite.

Kwa kuwa Wewe ni kijito cha faraja yangu
 yote,
 U zaidi ya maisha kwangu,
 Ni nani niliye naye duniani ila Wewe?
 Au ni nani Mbinguni ila Wewe?

¹⁸⁴ Amina. Yeye alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, alikuwa Mungu. Naam, bwana. Martha alishikilia mpaka akapata kile alichoomba.

¹⁸⁵ Hapa ninii michache, yapata mwaka mmoja uliopita, siku moja nilikuja kutoka mikutanoni, nimechoka. Nilishuka kwenda kuzungumza kwenye maskani ndogo, mwanamke fulani, huenda ameketi hapa usiku wa leo, kama yuko, ninamtaka asimame, alikuwa ametoka hapa California mahali fulani, walikuwa wamemleta humo, alikuwa na uvimbe uliotokeza nje namna *hii*. Huo uvimbe ulikuwa na uzito wa ratili hamsini ama sitini, alikuwa tamasha mbaya sana. Ilibidi wanaume wamwingize ndani.

¹⁸⁶ Kwa kawaida maskanini ninachoka sana, siwaombe wagonjwa, ninaingia tu, nazungumza na kanisa, kisha narudi. Kama sijakosea, baadhi ya hao ndugu wameketi hapa usiku wa leo, kote kutoka Jeffersonville walioshuka kuja huku, waliosaidia kumbeba huyo mwanamke kote. Walisema. . .Nikatoka kupitia mlango wa nyuma. Alishikilia. Wakamwambia, wakasema, “Ndugu Branham hawaombe wagonjwa anapoingia namna hii, amechoka sana, hatumwiti. Ngojea siku chache.”

Akasema, “Siwezi.”

¹⁸⁷ Na kwa hiyo, akawauliza baadhi ya mashemasi, ama wadhamini, wampeleke nje kwenye mlango mdogo wa nyuma. Baada ya kumaliza kuzungumza, nikatoka nje, akanishika mguuni; akashikilia. Nikamwekea mikono, ndipo miezi michache kuanzia wakati huo yeye. . .Huyu hapa nje. . .Huyu ni wewe, dada? Huyu hapo amesimama sasa hivi. Hakuna hata ishara moja, njia moja, mahali popote hata kidogo. Ule uvimbe uliyeyuka nilipomwomba. Mungu alimponya mwanamke huyo, wakati ilibidi kundi la wanaume kumbeba na kumtoa nje.

188 Ilikuwa ni kitu gani? Kushikilia, kung'ang'ania, aliamini, naye akalishikilia, hilo ndilo linalohitajika. Inahitaji kitu fulani kung'ang'ania, kitu cha kushikilia.

189 Ilikuwa ni Mikaya huko chini wakati Yehoshafati na Ahabu . . . Mtu wa Mungu angetaka nini kufanya mapatano na mnafiki kama huyo? Aliingia katika kundi baya, kama tu watu wengi wafanyavyo, kuingia miongoni mwa wasioamini, Injili ya kijamii, upuuzi kama huo, nawe unajichafua. Yehoshafati akasema, "Inatupasa kwenda Ramoth-gileadi?"

"Mbona, hakika, kwa kawaida."

Wote . . . Walipanda na kuwachukua manabii mia nne waliolishwa vizuri, waliofunzwa, wakaja kule juu, nao wakasema, "Kwea, Bwana yu pamoja nawe."

190 Hezekia akaenda na kujitwalia pembe kubwa mno na kusema, "Kwa hizi utawasukuma watoke. Kwa sababu gani? Yoshua aliigawa hii nchi, na Ramoth-gileadi ni mali yetu." Ilisikika sawa, mnaona, ilisikika ni hoja nzuri, ya kimsingi. Kasema, "Utawasukuma tu moja kwa moja watoke nchini."

191 Mwajua, lakini kuna kitu fulani kanisani, moyo wa—wa mtu, ambaye ni mtu wa Mungu. Yehoshafati akasema . . . Angalieni pale, kuna mia nne wao, na wote kwa moyo mmoja, wakitoa sauti moja. Kasema, "Sasa, najua ya kwamba . . ."

192 "Hilo halina budi kuwa sahihi," Ahabu akasema. "Sasa, sisi ni Wayahudi," Yezebeli kwenye kiti cha enzi pamoja naye. Mnaona? Kasema, "Sasa, angalieni pale, manabii mia nne wa Kiyahudi wakisema, "Kwea, BWANA ASEMA HIVI."

Lakini hiyo haikusikika kuwa sawa. Yehoshafati akasema, "Hivi huna mmoja zaidi?"

"Mmoja zaidi? Ninahitaji nini na mmoja zaidi, wakati tuna seminari nzima hapa, askofu na wote? Tunahitaji nini na mwingine zaidi?"

"Vema," akasema, "hivi hakuna mmoja zaidi?"

Kasema, "Naam, kuna mmoja zaidi, lakini ninamchukia."

"Loo," Yehoshafati akasema, "mfalme asiseme hivyo. Nendeni mkamlete."

Kasema, "Yeye ni—yeye ni Mikaya mwana wa Imla," kasema, "lakini ninamchukia, daima anatabiri mabaya dhidi yangu, daima ananiambia jambo fulani."

193 Loo, naam, anakata mahindi, anaondoa vivimbe. Mnaona? Kila mtu anataka kubembelezwa na kupapaswapapaswa. Hiyo ndiyo sababu inafanya mimea ya tuta, haina budi kunyunyiziwa *hiki* kizuri, na *kile* kizuri. Ukristo ni mgumu. Injili inapaswa kushikwa kwa mikono mitupu, sio kwa glavu za kikanisa, kweli, glavu nyeupe nyororo, hizo ni za wanawake, si za wahubiri, la. Sikiliza, ndugu, Neno halina budi kutolewa jinsi tu lilivyo hapo,

si likiwa na fundisho fulani la sharti la seminari ndani Yake, bali jinsi tu lilivyoandikwa hapa.

¹⁹⁴ Kwa hiyo ninii... wakatuma halmashauri ya mashemasi kule, na kumwambia, kasema, “Sasa, angalia, Mikaya, tutakurudisha kwenye shirika kama tu utasema jambo lile lile askofu na hao wote wasemalo.”

¹⁹⁵ Alikuwa akizungumza na mtu tofauti hapo, Mikaya alijua kumtumainia Mungu ni nini. Akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, nitasema tu yale atakayoweka kinywani mwangu.” Loo, ndugu, jamani! Iwe ni seminari au si seminari yoyote, ushirikiano au hakuna ushirikiano, kasema, “Nitasema tu yale Mungu anayoweka kinywani mwangu.” Alichukua usiku huo kisha akarudi kesho yake, akasema, “Kwea, lakini nimewaona Israeli wametawanyika kama kondoo wakiwa na mchu-... , ama, bila mchungaji.”

Na kwa hiyo askofu huyu mkubwa akampiga kofi mdomoni na kusema, “Roho wa Mungu alipitia njia gani alipotoka ndani yangu?”

¹⁹⁶ Kasema, “Nilimwona Mungu ameketi Mbinguni, baraza likafanywa. Ndipo nikaona pepo mchafu akitokea, pepo wa uongo, akasema, ‘Nitashuka na kuingia katika kinywa cha hao manabii na kuwafanya watabiri uongo.’”

¹⁹⁷ Unasema, “Vema, sasa, ndugu, mtu angeweza kujua kama alikuwa amekosea?” Kwa nini? Ono la Mikaya lilikuwa ni kulingana na Neno. Neno la Mungu lilikuwa tayari limenenwa na—na nabii, nalo Neno la Bwana daima humjia nabii. Na kama nabii Eliya alikuwa amemlaani Ahabu na kumwambia ya kwamba mbwa watairamba damu yake, angeweza kubariki kile Mungu alichokuwa amelaani? Kwa hiyo ono lake lilikuwa kulingana na Neno.

¹⁹⁸ Mtu fulani aliniandikia barua hivi majuzi, akasema alikuwa katika huduma ya ukombozi, kasema, “Unaweza kujua kama ni Mungu anayesema nawe, ama—ama ni ibilisi?” Hmm, hmm!

Nikasema, “Lichunguze kwa Neno, kama haliambatani na Neno, basi limekosea, sijali linaonekana zuri jinsi gani.”

¹⁹⁹ Katika Agano la Kale walikuwa na njia ya kujua wakati nabii alipokuwa akisema kweli, ama mwotaji alikuwa akiota sawa. Walimpeleka hekaluni na kumweka mbele ya Urimu na Thumimu, na kama hizo Urimu na Thumimu zilifanya kazi, na msongamano huo wa nuru kama upinde wa mvua unamulika kutoka kwa hizo, Mungu alikuwa akimtambua nabii huyo kuwa ni kweli, ama unabii, ama mwotaji, lakini kama halikufanya hivyo, haidhuru lilionekana halisi jinsi gani lilikuwa ni kosa. Daima lilijibu, Mungu aliwapa mambo ya kimbinguni.

²⁰⁰ Nawaambia kwamba ukuhani huo ulimalizika, na kwamba Urimu na Thumimu iliinuliwa, bali tuna Mpya siku hizi, na

hiyo ni Biblia hii. Kama mhubiri, ama mtu mwingine yeyote, akihubiri fundisho lolote la sharti ama chochote nje ya Biblia hiyo, kwangu mimi ni kosa, si jinsi linavyoonekana halisi (lazima iwe ni kosa), halina budi kuambatana na Biblia hiyo. Um-hum! Usichanganye chochote Nalo, liache tu jinsi lilivyo, hivyo ndivyo Mungu ameliweka, na hivyo ndivyo tunavyopaswa kulikubali na kuliadini, naam.

²⁰¹ Yule kipofu, hakika, asingeweza kubishana nao theolojia, bali alishikilia, alijua ya kwamba wakati mmoja alikuwa kipofu halafu angeweza kuona. Hakika. Alijua jambo hilo moja, alishikilia sana. Walisema baba na mama yake. . . Wao walisema, “Mtu yeyote anayemkiri nabii huyu wa Galilaya, tutamfukuza kanisani.”

²⁰² Na kwa hiyo jamaa huyu alikuwa ameshika kitu fulani. Jambo fulani lilikuwa limemfanyikia, naye alishikilia, angeweza kuwaambia. Sasa, asingeweza. . . Akasema, “Ni jambo geni kwangu sasa, kwamba hili hapa jambo ambalo Mungu pekee angeweza kufanya, wala halijatendeka katika lolote la makanisa yetu kote katika nyakati nijuazo, mtu aliyezaliwa kipofu anapata kuona. Nanyi mnadhaniwa kuwa ndio viongozi wa watu wa siku hizi, na hata hivyo hamjui alikotoka? Ni jambo la kushangaza.”

²⁰³ Ndugu, alikuwa na hoja nzuri sana za kubishania pale, nafikiri. Naam, bwana. Nao watu wanasema leo hii, “Haya yote yanahusu nini?” Wala sijui, wanatheolojia, na kadhalika, ya kwamba Biblia inabashiri jambo lili hili kutukia. Loo, ndugu, jinsi tunavyopaswa kushikilia!

²⁰⁴ Filipino, aliposimama pale na kumsikia Yesu akizungumza na Simoni, na kumwita Simoni, kasema, “Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona,” wala kamwe hakuwa amemwona hapo awali, alishikilia sana. Akamshika Nathanaeli, na wakati Nathanaeli alipokuja, Yeye alisema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!”

Akasema, “Ulinijua lini Wewe, Rabi?”

Kasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.”

Akaingia kushikilia sana, akasema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.”

²⁰⁵ Maskini yule mwanamke kisimani, alikuwa akimtazamia Masihi kuja. Alikuwa amewasikia wanatheolojia wote na huku na huku, naye akawazia afadhali atembe mtaani na awe kahaba, kama hiyo ndivyo bora zaidi waliyokuwa nayo.

²⁰⁶ Naye, siku moja, alishuka akaja kisimani kuchota maji, huyo hapo ameketi Mtu wa kawaida, akionekana mwenye umri wa kama miaka hamsini, nadhani. Akamtazama, Naye akamwomba

ampe maji anywe, naye akaingilia desturi na kusema, “Kuna ubaguzi,” na kadhalika.

Lakini aliposema, “Nenda, kamwite mume wako, mje naye hapa.”

Alisema, “Sina mume.”

Kasema, “Umeseema kweli. Ulikuwa na watano, naye uliye naye sasa siye mume wako.”

Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Tunajua ajapo Masihi, mambo haya yatakuwa ndiyo atakayofanya.”

Akasema, “Mimi ninayeseema nawe Ndiye.”

²⁰⁷ Sasa, hakupaswa, kulingana na sheria, kumwambia mwanamume chochote sokoni, kwa sababu alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya, lakini, ndugu, alikuwa ameshikilia, naye akawashawishi katika uvumilivu wake hata akasema, “Njoni, mwone Mtu, msikae *hapo*, msikae *hapa*, njoni mwone Mtu ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi aliyeahidiwa? Kasema ‘Bwana Mungu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.’ Msikieni.” Alishikilia mpaka akawaleta hao watu huko nje, nao wakaliadini.

²⁰⁸ Inanikumbusha juu ya hadithi ndogo tuliyokuwa nayo huko Meksiko, ambapo *Sauti* ya Wafanyabiashara Wakristo ilikuwa na makala yake hapa si muda mrefu uliopita. Tulishuka kule na . . . Jemadari Medina ndiye aliyenipeleka kule chini. Na kwa hiyo wakapata shida kidogo kuhusu serikali ya Meksiko kumleta Mprotestanti, na kwa hiyo, kwa kikosi hiki cha kijeshi, na kwa hiyo askofu akaenda na kusema, “Bwana,” kasema, “je, unajua mtu huyu si Mkatoliki?”

Akasema, “La, lakini,” kasema, “nakisia yeye ni mtu mwenye sifa nzuri, maelfu wanakuja kumsikiliza akihubiri, wanasema.”

Akasema, “Loo, ni wale tu wasio na elimu wala maarifa wanaotoka kwenda kumsikia mtu kama huyo.”

Kasema, “Mmekuwa nao huku chini kwa miaka mia tano, kwa nini hawana elimu wala maarifa?”

Nadhani huko kulikuwa ni *kunyamazisha* kuzuri. Na kwa hiyo walituruhusu kupata mahali huko nje, na maelfu wakakusanyika. Nami nilipaswa kuwa huko yapata siku tatu usiku.

²⁰⁹ Usiku mmoja jukwaani, niliangalia, na huyu hapa anakuja maskini ndugu wa Kimeksiko, kipofu kabisa, miguu yake mitupu na amejaa sugu mwili mzima, kofia yake kuukuu mkononi mwake, iliyoshonwa kwa kamba, miguu ya suruali yake imeraruka juu *kule*. Nikamwangalia, mwili wote umejaa mavumbi. Alikuwa akija pale ameshika kofia yake mkononi

mwake, alikuwa akigugumiza jambo fulani kwa mtu aliyekuwa akimleta. Alipofika karibu nami, aliingiza mkono mfukoni mwake na kutoa msalaba mdogo na kuanza ku—kusema ninii—“Salamu, Mariamu,” nilimfanya aiweke.

²¹⁰ Na kwa hiyo, akaja pale, nami nikamwangalia, nikawazia, “Huyu hapa, maskini jamaa mkongwe, labda kamwe hakupata chakula kizuri maishani mwake. Huyu hapo sasa, akiangalia, hana hata viatu mguuni, mimi hapa nimesimama na jozi nzuri ya viatu. Hapa nimesimama na suti.” Ninaamini ilikuwa ni suti ile ile ambayo Ndugu Carl Williams, mke wake aliyonipa, *pale*. Nami—nami nilikuwa nimesimama pale, nikawazia, “Hapa nimevaa suti.” Nilifikiri...Nikaweka mabega yangu... Nikawazia, “Kama litamtosha, hakika nitampa.”

²¹¹ Nikaweka miguu yangu kando ya yake, lisingemwenea hata kidogo, ndipo nikawazia, “Nifanye nini?” Nami nikawazia, “Huyo hapo anayumbayumba katika upofu, maskini jamaa mkongwe.” Huna budi kuwahurumia watu, la sivyo hutafaa kitu kuwaombea. Hivyo—hivyo tu. Nami nikawazia, “Kama baba yangu angaliishi, angalikuwa na umri kama huo.”

²¹² Nikamkumbatia kwa mikono yangu, na kuanza kumkumbatia namna *hiyo*, kisha nikasema, “Bwana Yesu, hakuna kitu kinachoweza kumsaidia ila Wewe. Hana hata senti moja ya pesa, na labda kamwe hajawahi kula chakula kizuri, wala kuvaa suti nzuri ya nguo maishani mwake. Naye huyu hapa amesimama, nayo maumbile yamekuwa katili sana kwake, mpaka hapa yeye ni kipofu. Angalia yale majaliwa yamemtendea. Ee, Bwana Mungu, uturehemu.”

²¹³ Nikamsikia akipaza sauti “Gloria a Dios!” Ndipo nikaangalia kote, mzee huyo aliweza kuona vizuri kama nilivyoweza. Huyu hapo akaondoka jukwaani akishangilia, akipiga makelele.

²¹⁴ Kesho yake usiku kulikuwako na lundo zima la shali kuukuu na makoti, yaliyolundikwa juu *hivi* jukwaani. Mvua ikinyesha...Sasa, hao watu hawakuja na kubishana kwa sababu nilikaa mpaka saa tatu, sikufika kule mpaka saa tatu. Nao walikuja pale saa mbili ama saa tatu asubuhi, na kuegemeana, wakiegemeana tu wao kwa...hakuna mahali pa kuketi, walisimama tu kwenye uwanja huu mkubwa na kuegemeana.

²¹⁵ Kwa hiyo nilipofika jukwaani, nikaanza kuzungumza juu ya imani, nikiangalia juu ya lundo hili kubwa la shali kuukuu...Jinsi walivyopata kujua ni za nani, na kofia, na makoti, na kadhalika! Nikaangalia chini kote kule. Ndipo Billy akanijia, kasema, “Baba, tuna mabawabu mia moja au zaidi wanaosimama kule chini, na kuna mwanamke aliyepiga na mtoto aliyekufa amesimama pale,” kisha kasema, “sisi... ”

wao...hatuna mabawabu wa kutosha kumzuia mwanamke huyo asingie mstarini.”

“Vema,” nikasema, “ana ukubwa gani?”

Naye akasema, “Vema, yeye ni kitu kidogo tu.” Kisha kasema, “Lakini amekuwa akisimama hapa siku nzima na mtoto huyo aliyekufa.”

²¹⁶ Naye Ndugu Jack Moore, wengi wenu mnamjua, alikuwa amesimama nyuma yangu, nikasema, “Ndugu Jack...” Ndugu Espinoza, wengi wenu watu wanaozungumza Kihispania mnamjua Ndugu Espinoza, naye akasema...alikuwa akinifasiria. Ndipo nikasema, “Ndugu Moore, nenda kule, yeye hanijui, nenda kule ukamwombee.”

²¹⁷ Naye angepitia kwa maskini mabawabu pale, angekimbia chini ya miguu yao, akapanda juu ya mgongo wao, ameshika mtoto mchanga aliyefariki mkononi mwake, maskini mwanamke Mkatoliki, naye alikuwa akijaribu kupanda kule juu.

²¹⁸ Ati nini? Imani chanzo chake ni kusikia. Alikuwa amesikia kwamba kipofu alipata kuona. Alijua kama huyo alikuwa ni Mungu, ilikuwa ni Mungu kwa walio hai, Mungu angeweza kuwafufua wafu. Ilikuwa ni Mungu yeye yule ambaye angeweza kuyafungua macho, angeweza kumfufua mtoto wake mchanga, haidhuru alikuwa katika hali gani. Jambo ndilo hilo. Alijua Yeye alikuwa ni Mungu, naye alikuwa akijaribu kupanda kule juu.

Na kwa hiyo, Ndugu Moore akaanza kwenda kumwombee mtoto huyo mchanga, nami nikageuka na kuanza kusema, “Na kama nilivyokuwa nikisema...”

Ndugu Espinoza akafasiri, “Imani ni ba-...”

²¹⁹ Ndipo nikaangalia na hapa mbele yangu kulikuwa na mtoto mchanga wa Kimeksiko, maskini uso mweusi, na ufizi mdogo ukimetameta, jamaa mdogo sana, akitabasamu tu, ameketi papa hapa mbele yangu. Nikawaza, “Huyo hana budi kuwa ni yule mtoto mchanga.” Nikaangalia kote, naye Ndugu Moore alikuwa akijaribu kushuka kupitia mabawabu, nikasema, “Hebu kidogo, Ndugu Moore. Ondokeni, enyi mabawabu.”

²²⁰ Sababu ya yeye kupanda juu, hakuwa na kadi ya maombi. Ndugu, nilimwita Mañana, ambalo linamaanisha “kesho,” alikuwa mwenda pole sana, angeshuka tu pale, na kusimama karibu, na kutoa kadi za maombi. Ndipo Billy akashuka kwenda kumwangukia, kuona ya kwamba hakuuza yoyote ya hizo, kwa hiyo, kuhakikisha ya kwamba aliendelea. Kwa hiyo asingeweza kuzungumza Kihispania. Kwa hiyo a—akasambaza kadi zote za maombi, wala hakuwa na zingine, naye alikuwa anaenda kufaulu kwa vyovyote vile. Alikuwa ameshikilia, alitaka jambo hilo lifanywe.

Na kwa hiyo, Ndugu Moore akaanza kurudi hivyo, na—nami nikasema, “Ngoja kidogo, Ndugu Moore.”

Akasema, “Kuna nini?”

221 Nikasema, “Sijui. Usifasiri, Ndugu Espinoza.” Nikasema, “Nilimwona maskini mtoto mchanga wa Kimeksiko amesimama akiniangalia moja kwa moja, moja kwa moja huko—huko juu ya kusanyiko papa hapa.” Nikasema, “Hebu aje huku.” Na kwa hiyo kamwe hawakufasiri hilo.

222 Ndipo maskini mama huyo akaja pale, maskini mwanamke mrembo, karibu, loo, ningesema mwenye umri wa miaka ishirini na mitano, amelowa maji kabisa, nazo nywele zake nzuri zikining’inia usoni mwake, nayo macho yake yamechomwa sana na machozi, na jinsi michirizi hiyo ilivyoshuka usoni mwake. Ndipo akakimbia pale, akaanguka sakafuni, akaanza kupiga mayowe, “Padre.” Nafikiri linamaanisha, “Baba.” . . . ? . . . Padre? Na “Padre,” daima . . . namna hiyo.

Na—nami nikasema, “Simama, simama.” Ndipo Ndugu Espinoza akaja pale, nikasema, “Mtoto huyo alikufa lini?”

223 Akasema, “Saa tatu asubuhi ya leo.” Na hiyo ilikuwa yapata saa nne na nusu usiku huo. Na amelowa maji tu kama . . . Lile blanketi dogo lililowekwa juu namna *hiyo*, alikuwa na umbo dogo, ameishikilia namna *hii*.

224 Kasema, “Tulia tu, kwa dakika moja.” Na—na kwa hiyo akasimama, nami nikasema, “Baba wa Mbinguni, nilimwona katika ono mtoto mchanga wa Kimeksiko, sijui ni mtoto huyu mchanga au siye, lakini kutuliza moyo wa mama huyu, na hilo lingeweza kuwa ni ono kutoka Kwako, hiyo ndiyo sababu niko hapa, ninaweka mikono yangu juu ya . . .” maskini mtoto huyo mchanga akafanya, “Waaah, waaah,” akaanza kurusha miguu yake midogo namna *hiyo*, huyo hapo hai. Niambie ni kwa nini. Kushikilia kwa mwanamke.

225 Huenda Ndugu Espinoza ameketi hapa usiku wa leo. Kuna wengi . . . Hiyo ni kweli? Ndugu Espinoza yuko humu ndani? Yeye ni . . . Ninyi nyote mnamjua, nanyi mnaweza . . . mnaijua hadithi hiyo. Ilikuwa ni kitu gani? Maskini mwanamke huyo, akishikilia. Loo, alijua kama Mungu angeweza kuyafungua macho ya kipofu huyo, angeweza pia kumponya mtoto wake mchanga, kumfufua.

226 Na kwa hiyo nikamwambia Ndugu Espinoza, “Usiseme lolote kuhusu hilo. Usifanye hivyo sasa, maana kitu pekee nilichoona kilikuwa ni mtoto tu pale, sijui maana yake. Wewe mtume mkimbiaji pamoja na huyo mwanamke, na uende kwa huyo daktari, na kupata taarifa ya kwamba huyo mtoto mchanga alikufa, naye akamtangaza kuwa amekufa.”

227 Ndugu Espinoza akamtuma mkimbiaji pamoja naye, naye akaenda kesho yake kwa daktari, daktari akasema, “Nilimtangaza huyo mtoto kuwa amekufa jana asubuhi, alikufa kwa nimonia,” ama kitu kama hicho, “saa tatu. Mtoto alikuwa amekufa, na sasa yu hai.” Haleluya! Kwa nini? Imani hiyo.

Ingawa alikuwa Mkatoliki, nilikuwa Mprotestanti. Imani ilishika kitu fulani. Haleluya!

²²⁸ Inakubidi kushikilia, kung'ang'ania, inakupasa kujua ya kwamba Mungu angali ni Mungu, na Mungu daima alikuwa ni Mungu, Mungu daima atakuwa Mungu. "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Ishike kwa imani na ung'ang'anie, usiliachilie, Mungu aliliahidi, ni juu ya Mungu kuliweka sawa. Mungu alitoa ahadi, Mungu ataitimiza.

²²⁹ Na tuinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Sitamalizia hili mpaka wakati mwingine kwa sababu ni—ni... Iitokea niliona inachelewa kidogo. Kushikilia, kung'ang'ania... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁰ Kesho alasiri nitatenga alasiri nzima kuwaombea watu walio na kadi za maombi. Ninajisikia tu kwamba Roho Mtakatifu yupo hapa, nanyi mna imani ya kutosha kumfanya atende kazi. Mnaamini hilo? Inueni mikono yenu kama mnaamini. Vema. Inahitaji hiyo kumshusha Roho.

²³¹ Simwoni mtu mmoja ninayemjua katika kusanyiko hili, ni yule mwanamke tu aliyeshuhudia sasa hivi hapa, akasimama, ambaye aliponywa huo uvimbe mkubwa.

²³² Na kama sijakosea, nilitaka kuuliza hili jana usiku, huyu si ni Dada Upshaw aliyeketi hapa? Mungu akubariki, Dada Upshaw. Mumewe, nyote mnamkumbuka Ndugu Willie Upshaw, alikuwa kwenu usiku huo, mgonjwa kwa miaka sitini na kitu kwenye kiti cha magurudumu, Mungu akamponya, naye akaponywa mpaka alipoenda kuwa pamoja na Yesu miaka kadhaa baadaye. Nje ya huyo, hao tu ndio niwajua.

²³³ Lakini una haja na Mungu. Sasa, hebu tusimame tu, tuchukue tu dakika moja kusoma kwa dakika moja. Sasa, ni wangapi wenu hapo wanaojua ya kwamba Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, wakati alipokuja, Yeye alikuwa ni Masihi wa Mungu, Mtiwa Mafuta? Mnaamini? Watu walijuaje Yeye alikuwa ni Mtiwa Mafuta? Kwa sababu alifanya ishara ya Masihi. Sasa, hawakuwa na nabii kwa muda wa miaka mia nne, na Israeli daima huwaamini manabii wao.

²³⁴ Biblia inasema, "Akiwapo mtu miongoni mwenu aliye wa rohani au nabii, mimi Bwana nitajitambulisha kwake, na kusema naye katika maono," na kadhalika. "Na kama yale asemayo yakitimia basi msikieni, lakini kama hayatimii basi msimwogope nabii huyo, kwa maana sijasema naye." Vema, hiyo ni akili tu, mnaona, kwamba ingekuwa.

²³⁵ Sasa, Masihi, kulingana na Biblia, alikuwa awe Nabii, Mungu-Nabii. Musa alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii," katika Kumbukumbu la Torati, "kama nilivyo mimi." Basi alipokuja, walimtambua je kuwa ni Nabii? Kwa sababu Yeye alitabiri mambo yaliyokuwa kweli kabisa, Yeye alijua mawazo yaliyokuwa moyoni mwao,

aliwaambia wao walikuwa ni akina nani, walikuwa ni nani, mahitaji yao yalikuwa yapi, yale waliyokuwa wamefanya. Hiyo ni kweli? Nao walijua hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi.

Filipo alisema, “Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli,” alipomwambia habari zake, mwujiza ulipofanywa juu yake.

²³⁶ Sasa, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 14, na kifungu cha 12, Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.”

²³⁷ Sasa, kama niliwaambia usiku wa leo. . . Hebu niwaonyeshe kuhusu udhaifu wa hali ya kanisa. Tunadai kuwa Wakristo. Kama nilisema roho ya John Dillinger ilikuwa ndani yangu, ningekuwa na bunduki na ningekuwa mhalifu, maana hiyo ni katika maumbile. Kama nilisema roho. . . Ukiweka uhai wa—wa mmea wa boga katika mzabibu, utazaa maboga. Hakika, uhai uliomo ndani yake ndio unaoutoa. Hebu weka uhai kutoka kwa mtofaa ndani ya mpeasi, utazaa matofaa, maana uhai wa mtofaa uko ndani yake.

²³⁸ Weka Uhai wa Kristo katika mtu binafsi, utazaa matunda ya Kristo, na Uhai wa Kristo. Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Sasa, angalieni, je, Yeye aliwahi kuandaa shule, seminari? “Kazi nizifanyazo. . .” Yeye alisema, “Msiponiamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo, zinanishuhudia Mimi.”

²³⁹ Ni matendo gani yaliyomshuhudia? Mwangalieni maskini mwanamke huyo kule juu, akasema, “Ninajua ajapo Masihi atafanya mambo haya, lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

²⁴⁰ Akaingia na kusema, “Je, haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Hivyo sivyo Masihi anavyopaswa kufanya? Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya.” Mnaona?

²⁴¹ Vema, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye ni yeye yule. Sasa, jambo pekee ni ule mwili wa kawaida. “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu,” kosmosi, utaratibu wa ulimwengu, “hautaniona tena. Hata hivyo ninyi mtaniona,” Kanisa, mwaminio, “kwa kuwa mimi” na *mimi* ni kiwakilishi nafsi, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari,” ukamilifu. “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, hata milele.” Basi kama Roho wa Kristo yuko ndani yetu, Yeye atafanya kazi za Kristo. Hapo ndipo imani yangu inaposimama.

²⁴² Nanyi mnajua mimi si mhubiri, sina elimu, siwezi kuhubiri, sidai kuwa. Lakini kuhubiri kwangu ni kwa karama, thibitisho la yale wahubiri wanayohubiri. Katika ujinga wangu, nadhani Mungu aliniacha tu nilelewe namna hiyo bali aliujuua moyo

wangu, kwamba ninawapenda watu na kumpenda Mungu, ninataka kufanya jambo fulani.

²⁴³ Na kama siwapendi ninyi, basi simpendi Mungu. Njia pekee ninayoweza kumtumikia Mungu ni kuwatumikia ninyi. “Tumikianeni. Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, mlinitendea Mimi.”

²⁴⁴ Nina shughuli gani hapa nje usiku wa leo? Nini... mbona siko nyumbani? Kwa nini siko juu vilimani pamoja na ufito wangu wa kuvua samaki mahali fulani? Ati niwe huku chini nikiwa mdanganyifu na kwenda kukutana na Mungu huko ng'ambo katika Hukumu? Si mimi. Nitaenda kuvua samaki, niende kuwinda kwanza, na kukutana na Mungu kwa amani. Ati nisimame hapa pamoja na mdanganyifu... .

²⁴⁵ Sio umaarufu, mnajua ninaepuka jambo hilo. Sina mipango mikubwa, na kuwaomba watu pesa, na—na upuuzi huu wote wa namna hii, kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu. Ninaweka mkutano wangu ambapo ninaweza kwenda popote Mungu anitumapo, kama ni, haidhuru kama ni Timbuktu, ama popote pale. Kama akitaka niwahubirie laki tano, kama vile huko Bombay, Yeye huntuma kule, mtu mwingine huidhamini. Nikitaka kwenda huku chini ambako kuna watu wanne ama watano tu, si lazima niwe na pesa zozote. Ninataka kuwa mahali ambapo Mungu anaweza kunitumia. Na kila mmoja wetu hapa ndani, tunataka tu kuwa mahali ambapo Mungu anaweza kututumia. Mnaona?

²⁴⁶ Sasa, Yeye ni Mungu. Na kama Yeye si Mungu yeye yule leo ambaye Yeye alikuwa daima, basi Yeye kamwe hakuwa Mungu. Nayo Biblia inasema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu. Hiyo ni kweli? Naye ni, anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, Kuhani Mkuu aliye hai, anayeishi daima, kutuombea, na anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

²⁴⁷ Sasa, ushuhuda wa Bibi Shakarian, mamia ya wengine, wanaweza kushuhudia jambo lile lile. Sasa, mnajua ya kwamba mimi si Masihi, mimi ni ndugu yenu, aliye mdogo kuliko wote miongoni mwenu. Nilikuwa mhubiri wa Kibaptisti nikija miongoni mwenu enyi watu, kwa sababu Wabaptisti wasingeupokea, nao wakaniambia nilikuwa nimerukwa na akili. Lakini najua kama Mungu alituma, kuna mtu fulani mahali fulani kuupokea mahali fulani, kwa hiyo hiyo ndiyo sababu niko hapa.

²⁴⁸ Sasa, ni karama tu, kama Mungu ataniweka tu mahali hapo, mimi ni msemaji Wake tu. Sasa, watu hawa ni wasomi, wana mafunzo, wanajua jinsi ya kuyaweka pamoja, inanibidi tu kulitapanya huko nje kwa njia yoyote, kwa uvuvio tu. Lakini wanajua jinsi ya kuyaweka pamoja na kuyafanya yawe na maana, bali inanibidi tu kunyoosha mkono, na kulichukua, na

kulitupa tu, na kulifikia, kulichukua, na kulitupa; ndiyo njia pekee niliyo nayo ya kufanya jambo hilo.

²⁴⁹ Lakini katika hii, karama, kama Mungu ataijalia, kwamba Yeye achukue na kutenda kazi, na kunena kupitia hapa, Kuhani Mkuu yeye yule tu. . . Yule mwanamke aligusa vazi Lake. . . Na kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, yeye yule jana na hata milele, atatenda vivyo hivyo kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule. Mnaamini hilo? Sasa, mwaminini Mungu. Msitie shaka, bali aminini tu.

²⁵⁰ Ninataka kujua, hapa, ninyi watu mlio wagonjwa, popote humu jengoni popote ulipo, na unajua ya kwamba sijui hata jambo moja kukuhusu, inua tu mkono wako. Vema, ni wote tu. Sasa, wewe omba na ufanye hivi. . .

²⁵¹ Sasa, hili liliahidiwa. Kama ningalikuwa na wakati wa kuwarudisha mahali ambapo Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za—za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu. . .” Hivi mliona ni Kanisa la namna gani yule Malaika aliketi karibu nalo, wakati alipokuwa ameuelekeza mgongo Wake kwenye kusanyiko, ama, kurudi hemani na kusema, “Kwa nini Sara akacheka?” hemani?

²⁵² Sasa, Yesu anatabiri papo hapo ya kwamba jambo hilo litatukia tena. Ni. . . Mungu alijithibitisha Mwenyewe hivyo kwa Wayahudi, kwa Wasamaria, bali si kwa Mataifa, maana Mataifa hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote. Leo tunamtazamia Masihi, na jinsi alivyofanya huko nyuma, Yeye, Mungu ni Mungu, kamwe havezi kufanya uamuzi na halafu abadilike, na kusema, “Nitafanya jambo lingine.” Na kama akiliacha Kanisa liingie kwa theolojia tu, bila kujionyesha Mwenyewe wazi miongoni mwao namna hiyo, basi Yeye anawafanyia jambo fulani huko nyuma hakutufanyia sisi. Lakini Yeye aliahidi kufanya hivyo, hilo ndilo ninaloamini, na hilo ndilo analothibitisha.

²⁵³ Sasa, mwaminini Mungu. Shikilieni. Useme, “Bwana Yesu, maskini mhubiri huyo mwenye upara aliyesimama hapo hajui lolote kunihusu mimi, bali Wewe unajua. Bwana Yesu, pasipo kuwa na wasiwasi, kushinikizwa kabisa, naja kwa unyenyekevu, ninakiri kila dhambi niliyowahi kufanya. Nakupenda, Bwana. Hebu nikuguse Wewe, utanijalia, Bwana? Ninakuhitaji. Basi Wewe tumia midomo yake, kama ameniambia kweli, nami ninaamini ameniambia, tumia midomo yake na kujibu, Baba wa Mbinguni, na kunjulisha. Nena nami kama ulivyosema na yule mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu, nitakuamini Wewe.” Utafanya hivyo? Ingekufanya ushikilie basi, kwamba ushikilie moja kwa moja? Vema. Na tuombe.

²⁵⁴ Sasa, Baba wa Mbinguni, mkutano ni Wako. Siwezi kujifanya. . . Ninaomba tu, Bwana, hata sikuombi ufanye hivyo, bali ikiwa ni katika mapenzi Yako ya Kiungu, katika utaratibu Wako, na itimie. Haidhuru ningesema nini, Neno moja kutoka

Kwako litamaanisha zaidi ya yale sisi sote tungeweza kusema, Bwana, maishani, Neno moja tu kutoka Kwako.

²⁵⁵ Sasa, nimejaribu kupitia miaka hii thelathini na moja ya kuhubiri kulishikilia Jina Lako, kunena habari Zako. Na sasa, Baba, Wewe hujawahi kunipungukia wakati wowote, wala siamini utanipungukia usiku wa leo. Kwa hiyo ninaomba ya kwamba Wewe utatupatia kitu fulani, Bwana, ili watu waweze kwenda nyumbani, wageni pamoja nasi, na kusema, “Kweli, Yesu Kristo hajafa, Yeye yu hai, kwa sababu nimemwona akitenda kazi kupitia wanadamu usiku wa leo, akifanya kazi ile ile, kwa hiyo lazima iwe ni Uhai ule ule.” Ndipo watakuonea njaa, Bwana, na waje na kukukiri Wewe kama Mwokozi wao. Tujalie, naomba, katika Jina la Yesu. Amina.

(Wanavuta nyuma *hapa*, kamwe msifanye hivyo. Ombeni. Mnaona? Niombeeni tu. Mnaona? Na iwe *hapa* nje. Wakati wetu utakuwa kesho.)

²⁵⁶ Mnaketi ndani moja kwa moja upesi. Ninapenda hilo. Loo, hamjui jinsi ninavyojisikia! Jambo lingine, je, mmejninunulia picha Yake tayari? Ni wangapi waliowahi kuiona picha ya yule Malaika wa Bwana? Wanayo huko nyuma na mnaweza kuipata. Ilipigwa hapa, iko Washington DC, katika Ukumbi wa Sanaa wa Kidini, Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha, Nguzo ya Moto.

²⁵⁷ Miaka mingi iliyopita, nikiwa mvulana mdogo, nilipokuwa nikibatiza huko chini mtoni siku hiyo, ujumbe wangu wa kwanza tu katika kanisa la Kibaptisti la Kimishenari, nilikuwa nikibatiza mia tano. Na alasiri hiyo, Juni, 1933, Juni, yapata tarehe 15, hii hapa ikaja ile Nguzo ya Moto ikizungukazunguka kutoka angani, moja kwa moja katika alasiri nzuri, yenye jua kali, nayo ikashuka moja kwa moja chini kisha ile Sauti iliyoitikisa nchi nzima kule, ikasema, “Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kule Kuja kwa kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utakutangulia Kuja mara ya pili.” Sasa, hiyo ilianzisha uamsho mara baada ya hapo. Na hapo umeenea kote nchini, kote ulimwenguni, uamsho wa Pentekoste. Na hilo ndilo limetukia, kule kuja mara ya pili kwa Kristo.

²⁵⁸ Na sasa, magazeti yalitangaza habari hizo huko Canada. Ilikuwa kwenye makala, na kadhalika, na ikaingia kwenye Associated Press, niliendelea kuwaambia watu. Ndipo hatimaye jicho la kamera likaanza kuishika, na sasa wanayo huko nyuma.

²⁵⁹ Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba Nguzo hiyo ya Moto ilikuwa ni Yesu Kristo? Malaika wa Agano, hakika. Hakika. Sasa, angalieni, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, “Nilitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu.” Hiyo ni kweli? “Ninatoka kwa Mungu, naenda kwa Mungu.” Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Paulo, Sauli wakati huo, alikuwa

akienda zake Dameski kuwakamata baadhi ya watu waliokuwa wakipiga makelele kupita kiasi, wakipaza sauti na kuendelea.

²⁶⁰ Kwa hiyo alikuwa akienda zake, ndipo hiyo Nguzo ya Moto ikashuka mbele zake, watu hao hawakuiona, aliiona, hao waliokuwa pamoja naye hawakuiona, bali Nguzo ya Moto iliyompiga kwa upofu, naye akaanguka chini, ndipo akasema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

²⁶¹ Akasema, "Mimi ni Yesu." Alitoka kwa Mungu, Naye akarudi kwa Mungu. Na wakati Nguzo hiyo ya Moto, ile Roho, ilipokuwa katika mwili wa Mtu aliyelitwa Yesu Kristo, ilifanya miujiza hio. . .

²⁶² Naye ni yeye yule jana, milele. Nayo Hii hapa, ulimwengu wa kisayansi unathibitisha, kama George J. Lacy, mkuu wa FBI, aliyeichunguza ile picha, kama mjuavyo, hayo hapo maandishi yake yameambatanishwa nayo namna hiyo, alisema, "Nimekuwa mkosoaji wako, Bw. Branham, lakini," kasema, "jicho la kimitambo la kamera hii halitapiga picha saikolojia." Akasema, "Hiyo Nuru iliigusa lenzi."

²⁶³ Sasa, basi kama Roho huyo hatoi ushuhuda ule ule ambao Yesu Kristo anashuhudia, basi si Roho yeye yule, bali kama akitoa, ni Yeye miongoni mwetu. Je, unaweza kuamini kwa moyo wako wote?

²⁶⁴ Ombeni, mtu fulani katika sehemu hii hapa, ombeni tu na mtazame huku. Amini kwa moyo wako wote sasa. Roho Mtakatifu yupo hapa. Ninachukua kila roho hapa ndani chini ya mamlaka yangu katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Tulieni sasa, magonjwa haya yataenda kutoka mmoja hadi kwa mwingine, mnajua hilo. Ombeni tu.

²⁶⁵ Naam. Angalieni hapa, hivi hamwoni hiyo Nuru moja kwa moja juu ya mtu huyo aliyeketi hapo chini, Nuru ile ndogo inayowaka juu ya mtu ambaye ameinamisha kichwa chake. Ana ugonjwa wa mgongo, yuko tayari kufanyiwa upasuaji mgongoni mwake. Arthur, simama na upokee uponyaji wako katika Jina la Bwana Yesu.

²⁶⁶ Haleluya! Sasa, ninataka kuwaulizeni jambo fulani, ninataka kuwaulizeni ninyi ndugu: Aligusa nini? Kamwe hakunigusa mimi. Mnaona? Yuko yadi ishirini kutoka kwangu, kamwe hakunigusa mimi.

²⁶⁷ Kama hatufahamiani, tikisa tu mkono wako huku na huku, mtu huyo ambaye ndio kwanza aguswe na Mungu wakati huo. Kama hatufahamiani, utikise mkono wako.

Ati nini? Lakini Mungu alimjua.

²⁶⁸ Moja kwa moja chini ya ile safu kutoka kwake, pale, kuna maskini mwanamke mdogo wa Kimeksiko, mwembamba, anamwomba mumewe ambaye ana ugonjwa wa wasiwasi.

Amini, Dada, atakuwa mzima. Unaamini? Mungu akubariki. Sisi hatufahamiani pia. Kamwe usiwe na shaka, kuwa na imani.

Mnaona kile Yeye alichu? “Kinywa cha mashahidi wawili watatu kila Neno na lithibitike.”

²⁶⁹ Hapa, angalia pale, mwangalie mwanamke huyo. Kuna mwanamke mnene anayeketi pale. Ana ki—kidonda, kidonda kinachotokwa na damu mguuni mwake, kiko kwenye mguu wake wa kushoto. Naye alikuwa ameketi pale akiomba, “Bwana Yesu, na iwe ni mimi.” Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako huku na huku, namna hii.

²⁷⁰ Simjui mwanamke huyo, hatufahamiani. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako mama, kama hatufahamiani sisi kwa... Ningewezaje kujua anachoombea? Mungu yeye yule anayeweza kusikia maombi anaweza kujibu maombi...?... Yeye ni Mungu. Amina.

²⁷¹ Vipi kuhusu mwanamke huyu aliyeketi hapa amevaa gauni hili la kijani kibichi? Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Hatufahamiani, sivyo? Kama Mungu ataniambia shauku yako ni nini, utaamini? Unatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mpokeeni Roho Mtakatifu, Jina la Yesu Kristo.

Unaamini kwa moyo wako wote? Kuwa tu na imani, usiwe na shaka. Liamini Neno la Mungu. Uko tayari kuamini?

²⁷² Hapa, Hili hapa. Mtu huyu aliyeketi kwenye kiti hiki cha magurudumu. Bwana, naamini ulinijua. Kamwe siwezi kufanya hivyo. Lakini Nuru ilikuwa juu yako muda mfupi tu uliopita, endelea kuomba.

²⁷³ Mama, aliyeketi hapa, papa hapa mbele yangu. Ndio kwanza afanyiwe upasuaji, upasuaji kamili wa kuondoa mji wa mimba, tezi za kike. Haujafanikiwa vizuri, ni mbaya. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama mtumishi Wake? Unaamini? Unaamini ya kwamba Mungu anajua wewe ni nani kama ataniruhusu kulitaja jina lako? Bibi Cole, amini kwa moyo wako wote. Unaishi kwenye bloku ya 700 ya Mtaa wa Maple mashariki, Glendale, nenda nyumbani na uamini, naye Yesu Kristo anakuponya.

²⁷⁴ Jambo lingine, huyo ni mama yako aliyeketi moja kwa moja nyuma yako, naye anaogua. Hilo lilimfurahisha sana kuona binti yake ameponywa. Una uvimbe tumboni mwako *hapa*, unaoumbea. Unaamini kwa moyo wako wote? Basi utaponywa.

Aminini, iweni na imani.

²⁷⁵ Hii hapa juu ya mtu...?...Bwana. Una...?...U—utakufa kama ukiketi hapo, hivyo tu. Una ugiligili mapafuni mwako...?...

²⁷⁶ Mungu awabariki. Amina. Hebu tuseme, “Bwana asifiwe.” “Bwana asifiwe.”

Nitamsifu, nitamsifu,
 Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
 ajili ya wenye dhambi;
 Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
 Kwani Damu Yake imeosha kila . . .

Simameni kwa miguu yenu. Mpeni sifa kama mnataka kuponywa.

Nitamsifu, nitamsifu,
 Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
 ajili ya wenye dhambi;
 Loo, mpeni utukufu wote . . . (Yule pale akirudi.)
 Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

²⁷⁷ Je, unamtaka kama Mwokozi wako? Unaamini Yeye alipachukua mahali pako? Njoni madhabahuni sasa. Na tuombe, ninyi mnaomtaka Roho Mtakatifu, njoni huku . . . ? . . .

Nitamsifu, nita- . . .

Jambo ndilo hilo. Yuko hapa . . . ? . . . Njoo . . . ? . . . Hii ndiyo saa. Liamini.

Mpeni utukufu enyi watu wote,
 Kwani Damu Yake inaweza kuosha kila doa.

²⁷⁸ Njoo, rafiki mwenye dhambi. Njoni, ninyi msio na Roho Mtakatifu. Hii ndiyo saa ya kumpokea . . . ? . . . Huna budi kuja kujisalimisha.

Mtu yule pale mwenye TB, isahau, Bwana. Mungu alikuponya. Haleluya!

. . . Yeye utukufu enyi watu wote,
 Kwani Damu Yake imeosha kila doa.

Nitamsifu, nitamsifu,
 Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
 ajili ya wenye dhambi;
 Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
 Kwani Damu Yake inaweza kuosha kila doa.

Nitamsifu,


Bwana Yesu, jalia uponyaji huu katika Jina la Yesu.

Nitamsifu,
 Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
 ajili ya wenye dhambi;
 Mpeni utukufu enyi watu wote,
 Kwani Damu Yake imeosha kila doa.

Nitamsifu . . .

²⁷⁹ Endeeleni kupanda juu, endeeleni tu kupanda juu kila mtu anayemtaka Kristo. Roho Mtakatifu ndiyo kwanza ashuke juu ya mvulana mdogo hapa.

. . . msifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwani Damu Yake imeosha kila doa.

²⁸⁰ Baba wa Mbinguni, ninaomba sasa ya kwamba katika Jina la Yesu jalia ninii Yako . . . ? . . . Tujalie, Ee Mungu . . . ? . . . vitambaa hivi vya maombi, na uwaponye . . . ? . . . nami ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. 

62-0623 Anayeng'ang'ania
Great Western Exhibit Center
South Gate, California Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org